**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS

# FEDHA NA MIPANGO

**DKT. SAADA MKUYA SALUM (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO**

**NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**



**Mheshimwa Dk . Hussein Ali Mwinyi**
**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

**“Kila mtu unaponunua chochote ni wajibu wetu kudai risiti tena risiti ya mashine (EFD). Hiyo ndiyo itakayopelekea Serikali kuweza kupata kodi ya kufanya haya tunayoyafanya”**

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI ........................................................................................ 1

B. TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI ........................................ 3

C. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021- MACHI 2022. ........................................................................................ 5

a. Ukusanyaji Mapato Julai 2021 hadi Machi 2022 ........................................ 5

b. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ................................................ 6

c. Matumizi Julai 2021 hadi Machi 2022 .................................................... 6

d. Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu ...................................................... 7

e. Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu ...................................................... 7

D. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ........................................................ 8

E. TATHMINI YA DENI LA TAIFA ................................................................ 9

F. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/2022 ........................................................................................ 10

G. MAFANIKIO YA SERIKALI MWAKA 2021-2022 ........................................ 12

H. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022. ................. 23

I. SERA NA MIKAKATI YA SERIKALI ILIYOTUMIKA KWA MATAYARISHO YA BAJETI 2022-2023 ........................................................................ 23

I. HATUA ZITAKAZOCHUKULIWA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ................................................................ 24

J. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ..................... 29

a. Makadirio ya Mapato Serikali kwa mwaka 2022/2023 ................................ 29

b. Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 .......................................... 30

c. Hali ya Utegemezi kwa mwaka 2022/2023 .............................................. 32

K. SHUKRANI ........................................................................................ 32

L. HITIMISHO ........................................................................................ 33

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kuishuhudia siku hii adhimu katika historia ya Baraza letu la kumi. Hatimaye siku ya kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 imewadia, Hatua hii itawezesha Serikali kuendelea na hatua nyengine za kutekeleza shughuli zake za kuleta Maendeleo katika nchi yetu.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima, naomba kuchukua fursa hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa imani yake kwangu kwa kuniamini na kuniteua kushika nafasi ya kuwa msaidizi na mshauri wake katika masuala ya fedha na mipango ya nchi yetu nikiwa nashikilia nafasi ya Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango. Aidha, natanguliza shukrani zangu kwake kwa kumteuwa Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir kuwa Naibu Waziri. Kwa hakika Mheshimiwa Rais amefanya maamuzi sahihi kwa kumchagua Mheshimiwa Naibu Waziri ni muelewa na jasiri katika kazi. Hivyo, Mheshimiwa Naibu nakuomba tuendelee kushirikiana ili kufikia malengo ya Serikali yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukran maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake anazozichukuwa katika kuendesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kutupatia mashirikiano makubwa katika kutimiza mahitaji muhimu ya nchi na wananchi wake pamoja na jitihada anazozichukua kudumisha Muungano wetu. Kwa ujumla kazi zinazotekelezwa na Viongozi wetu hawa wakuu zimebeba dhana pana ya Utawala Bora. Viongozi hawa ni wasikivu na wepesi kuwafikia wananchi kuwasikiliza na kutafuta mbinu za kutatua changamoto zinazowakabili. Sote tumeshuhudia viongozi wetu wanavyokabili athari za Uchumi zinazosababishwa na matukio yasiyotarajiwa ikiwemo ugonjwa wa UVIKO-19 na vita kati ya Ukraine na Urusi, hii ni mifano thabiti ya kuonyesha kuwa Viongozi wetu hawa wana nia njema.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais wetu ambao ni Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Maasoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa jinsi wanavyojitolea na kujituma ili kufikia malengo ya Serikali na kuendelea kuwaunganisha Wazanzibar kuwa wamoja. Aidha, naomba niwashukuru Mawaziri wenzangu wote na kuwaomba tuendelee kushirikiana kwa karibu kuimarisha Umoja wetu ambao ndio chachu kwa maendeleo ya nchi yetu. Umoja wetu ndio ushindi wetu, na nina imani watu wasiopenda mshikamano wetu bado hawajaisha na hawatofurahia Maendeleo tunayoyapata. Tunachotakiwa kufanya ni kuendelea kushikamana ili hata watakapojaribu washindwe.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee napenda nikushukuru na kukupongeza wewe binafsi Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 ili nami niweze kutimiza wajibu wangu huo wa msingi Kikatiba. Lakini, shukrani zangu kubwa kwako wewe pamoja na Wasaidizi wako Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza hili kwa uongozi wenu mahiri na shupavu. Ukweli ni kwamba mnaendelea kuongoza vikao vyetu vizuri sana. Najua haikuwa kazi rahisi, penye wengi pana mengi, lakini kwa uhodari mkubwa nina imani tutakamilisha jukumu hili salama.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mara nyengine tena naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa michango na miongozo waliyotupatia wakati wa matayarisho ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022-2023 ambapo leo tunajumuika sote kwa pamoja katika uwasilishaji wa hotuba yetu. Aidha, nitumie fursa hii kuwaomba waendelee kuwa karibu nasi wakati tunapokwenda kutekeleza Bajeti yetu hii ili tufikie malengo ya Serikali yetu ya Awamu ya Nane.

7. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli ya matayarisho ya Bajeti ni mchakato ambao tulianza mbali na unahusisha wadau wengi. Nichukue fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali kutoka Serikalini na Taasisi zisizokuwa za Serikali (Taasisi za Dini, Vyama vya Siasa Asasi za Kiraia, Jumuia ya Wafanya Biashara) na wengine wengi kupitia Majukwaa ya Bajeti na warsha. Nawashukuru wote kwa mawazo na ushauri wao ambao umekuwa msaada mkubwa katika kukamilisha hotuba hii. Kipekee niwashukuru washiriki na wataalamu na ushauri wa masuala ya kodi kupitia vikao kazi vinavyohusu masuala ya mapendekezo ya hatua za kuimarisha mapato.

8. **Mheshimiwa Spika,** Kama ambavyo nimeeleza awali, uwepo wetu wa leo katika ukumbi huu ni sehemu ya kutimiza wajibu wetu kwa kukidhi matakwa ya Katiba yetu ya mwaka 1984 ya Kifungu cha 105 (kama ilivyorekebishwa) pamoja na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya namba 12 ya mwaka 2016. Vifungu hivyo vinatoa wajibu kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha kabla ya kumaliza mwaka wa fedha kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata wa fedha. Kwa kuwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 unakaribia kumalizika, Mapendekezo haya ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 yanawasilishwa ili kutimiza matakwa hayo ya kikatiba na kisheria.

9. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu lipokee Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022-2023. Aidha uwasilishaji wa hotuba ya Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022-2023 utawasilisha kwa pamoja na taarifa zifuatazo:

i. Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi;

ii. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2021- Machi 2022;

iii. Tathmini ya Utekelezaji wa hatua za Kuimarisha Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

iv. Tathmini ya Deni la Taifa; na


v. Matarajio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022.

## B. TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI

**10. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kupunguwa kwa maambukizi ya maradhi ya UVIKO-19 na kudhibitiwa kwa maambukizi mapya, uchumi wa Dunia umeanza kuimarika kwa kiasi kikubwa ukichangiwa na sababu mbali mbali zikiwemo kuimarika kwa uwekezaji na utalii, kufunguka kwa biashara na uzalishaji viwandani.


**Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi**

**2016- 2021**



11. **Mheshimiwa Spika**, Kasi ya Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar imeimarika na kufikia wastani wa 5.1% mwaka 2021 kutoka wastani wa 1.3% mwaka 2020. Ukuaji huo wa Uchumi kwa mwaka 2021.Sekta zilizoimarika zaidi ni sekta ya huduma kwa kufikia ukuaji wa 6.8 % kutoka -1.0% ya mwaka 2020 kulikotokana na kuimarika kwa shughuli za utalii; kuimarika kwa sekta ya fedha kufikia 9.9% kutoka 2.1%; kuimarika kwa shughuli za uwekezaji kulikopelekea kuongezeka kwa shughuli za ujenzi kufikia 8.9% kutoka 6.5%; na kuimarika kwa sekta ndogo za Umeme na Gesi kufikia 8.0% kutoka -2.8%.

12. **Mheshimiwa Spika,** Thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma imeongezeka hapa nchini na kufanya Pato halisi la Taifa kukua na kufikia thamani ya TZS 3.275 trilioni kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na thamani ya TZS 3.116 trilioni kwa mwaka 2020. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za soko (GDP at Current Prices) limefikia thamani ya TZS 4.633 trilioni mwaka 2021 kutoka thamani ya TZS 4.209 trilioni kwa mwaka 2020.




13. **Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumesababisha kuongezeka kwa Pato la Mwananchi na kufikia TZS 2.7 milioni ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 1,171 kutoka TZS 2.5 milioni sawa na Dola 1,099 kwa mwaka 2020. Kipato hiki kimeifanya Zanzibar iendelee kubaki katika nchi za uchumi wa kiwango cha kati cha chini (Low Middle-Income Status).

14. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imepungua na kufikia wastani wa 1.7% kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa 3.4% kwa mwaka 2020. Kupungua huko kumesababishwa na hatua za Serikali za kupunguza kodi za bidhaa za vyakula zikiwemo sukari, mchele na unga wa ngano kwa kiwango cha Dola 350 kutoka Dola 600 kwa kila tani moja. Aidha, Serikali imetoa bei elekezi za bidhaa mbalimbali zilizoingia nchini ikiwemo vyakula, bidhaa ya saruji na nondo.

15. **Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, kwa mwaka 2022 kasi ya mfumko wa bei imeanza kupanda na kufikia 2.8% mwezi wa Januari na 2.9% katika mwezi wa Februari 2022. Hii imetokana na kupanda kwa gharama za mafuta duniani kulikosababishwa na vita kati ya Urusi na Ukraine.

16. **Mheshimiwa Spika,** Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kufikia TZS 155.6 bilioni kwa mwaka 2021 kutoka TZS 65.7 bilioni kwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la 136.8%. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kufikia tani 6,775.5 zenye thamani ya TZS 115.3 bilioni kwa mwaka 2021 kutoka tani 3,506.8 zenye thamani ya TZS 38.3 bilioni kwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la 93.2% la usafirishaji wa zao hilo. Aidha, usafirishaji wa zao la mwani umeongezeka kufikia tani 12,611.1 zenye thamani ya TZS 11.9 bilioni mwaka 2021 kutoka tani 11,382.6 zenye thamani ya TZS 11.7 bilioni mwaka 2020. Kwa upande mwengine, uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka kutoka TZS 847.4 bilioni mwaka 2020 na kufikia TZS 968.6 bilioni kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la 14.3%.

## C. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI 2021- MACHI 2022.

### a. Ukusanyaji Mapato Julai 2021 hadi Machi 2022

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imekadiria kukusanya mapato ya jumla ya TZS 1,829.9 bilioni katika mchanganuo ufuatao: Mapato ya ndani ya TZS 1,134.9 bilioni; Mikopo ya hati fungani ni TZS 92 bilioni; Mikopo ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo TZS 220 bilioni; Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo jumla ya TZS 283 bilioni ikiwemo mikopo ya TZS 204 bilioni na TZS 79 bilioni Misaada; Misaada ya Kibajeti ya TZS 20 bilioni na marejesho ya TZS 80 bilioni ikiwa ni sehemu ya Ujenzi wa Terminal III kutoka Benki ya Exim ya China.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, mapato yaliyokusanywa yamefikia jumla ya TZS 1,127.82 bilioni sawa na 78% ya makadirio ya kukusanya TZS 1,449.40 bilioni kwa kipindi hicho cha tathmini na sawa na 62% ya Bajeti ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022. Uchambuzi wa Makusanyo hayo ni kama ufuatavyo:

   i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ilikusanya jumla ya TZS 256.36 bilioni sawa na 84% ya makadirio ya kukusanya TZS 306.72 bilioni kwa kipindi cha tathmini na sawa na 62% kwa makadidirio ya mwaka;

   ii. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), ilikusanya jumla ya TZS 275.18 bilioni sawa na 66% ya makadirio ya TZS 414.85 bilioni kwa kipindi cha tathmini na 52% kwa makadirio ya mwaka;

   iii. Makusanyo ya Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar, yalifikia TZS 13.30 bilioni sawa na 85% ya makadirio ya TZS 15.7 bilioni kwa kipindi cha tathmini na 63% ya makadirio ya mwaka;

   iv. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 130.90 bilioni sawa na 79% ya makadirio ya kipindi cha tathmini na sawa na 75% ya makadirio ya mwaka

ya kukusanya TZS 175.73 bilioni (ikiwemo Gawio la faida kutoka katika Mashirika ya SMZ la TZS 5.8 bilioni pamoja Gawio kutoka BOT ni TZS 9.0 bilioni);

v. Mikopo ya hati fungani ni TZS 100.00 bilioni sawa na 100% ya kipindi cha tathmini na 109% ya makadirio ya mwaka;

vi. Mikopo na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 349.76 bilioni sawa na 79.9% ya makadirio ya kupokea TZS 437.58 bilioni katika kipindi cha tathmini (inajumuisha TZS 230 bilioni za mkopo wa IMF); na 53.8 % kwa makadirio ya mwaka; na

vii. TZS 2.35 bilioni zimepokelewa kama General Budget Support (GBS) sawa 23.5% kwa kipindi cha miezi tisa na 12% ya makadirio ya kupokea TZS 20.0 bilioni kwa mwaka.

19. **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mapato kwa kipindi cha Julai /Machi umeambatanishwa katika **Jadweli namba I.**

**b. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022/2023, ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ilipangiwa kukusanya TZS 15.6 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa mapato yaliyokusanywa yamefikia jumla ya TZS 8.2 bilioni sawa na 52.5% ya kukusanya TZS 15.6 bilioni kwa mwaka.

**c. Matumizi Julai 2021 hadi Machi 2022**

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2021/2022, matumizi ya Serikali yamefikia TZS 867.60 bilioni sawa na 83% ya makisio ya TZS 1,041.55 bilioni ya lengo la kipindi cha tathmini na 47% ya lengo la matumizi ya mwaka ya TZS 1,829.91 bilioni. Matumizi hayo yamejumuisha:

i. Mshahara wa TZS 308.90 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo la kipindi cha tathmini na 70% ya makadirio ya TZS 441.70 bilioni;

ii. Matumizi ya kawaida ni TZS 85.03 bilioni sawa 58% ya makadirio ya kipindi cha tathmini, pia sawa na 42% ya makadirio ya mwaka;

iii. TZS 35.13 bilioni zilitolewa kama ruzuku za matumizi ya kawaida kwa Taasisi za Serikali ikiwa sawa na 53% ya makadirio ya kipindi cha tathmini na 36% ya makadirio ya mwaka;

iv. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 136.95 bilioni sawa na 93% ya makadirio ya Julai 2021-Machi 2022, pia sawa na 66% ya makadirio ya

mwaka. Uchambuzi wa matumizi haya unafuata katika aya nambari 23; na

v. TZS 301.61 bilioni zilitumika kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni 96% ya makisio ya kutumia TZS 314.48 bilioni kwa kipindi cha tathmini na 34.2% kwa mwaka ya kutumia TZS 882.81 bilioni.

22. **Mheshimiwa Spika,** Fedha za Serikali katika miradi ya Maendeleo ni TZS 88.97 bilioni; TZS 116.25 bilioni zilitotumika kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na TZS 96.39 bilioni ni fedha za mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha la Dunia (IMF).

### d. Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu

23. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 136.95 bilioni, sawa na 93% ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 147.98 bilioni zilitumika kwa huduma mbalimbali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi hayo yameelekezwa kulipia gharama zifuatazo: TZS 28.4 bilioni zililipwa Viinua mgongo kwa wastaafu 1,753 wa SMZ; TZS 23.5 bilioni zililipwa kama pencheni kwa wastaafu 14,707 kwa mwezi; TZS 28.3 bilioni zililipwa kwa marejesho ya Mikopo wa Ndani na Riba; TZS 16.98 bilioni zilizotumika kwa marejesho ya amana za wananchi 9,264 kati ya wananchi 10,317 waliopeleka fedha katika Kampuni ya Masterlife Microfinance ltd ambayo imefungwa kuendesha shughuli zake hapa Zanzibar; na TZS 39.9 bilioni zilitumika kwa matumizi maalum ya Serikali.


### e. Mfuko wa Miundombinu

24. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Miundombinu una lengo kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu nchini. Kwa kipindi cha miezi tisa, Mfuko ulikusanya TZS 14.29 bilioni ikiwa ni 63% ya makadirio ya TZS 22.86 bilioni kwa kipindi cha tathmini na 31% kwa makadirio ya TZS 46.47 bilioni kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa matumizi ya Mfuko umetumia TZS 3.15 bilioni zimetumika sawa na 7% ya makadirio ya mwaka na kugharamia miradi mitatu kati ya miradi tisa iliyopangwa kupatiwa fedha katika Mfuko huu.

f. **Misamaha ya Kodi iliyotolewa kwa Kipindi cha Julai 2021-Machi 2022**

**25. Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2021-Machi 2022, Serikali imetoa misamaha ya kodi yenye thamani ya TZS 25.4 bilioni ikiwa ni sawa na punguzo la asilimia 63.7 ikilinganishwa na misamaha iliyotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, Serikali imeunda Kamati maalum ya Kufuatilia na Kutathmini matumizi ya misamaha ya kodi ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha inayotolewa na Serikali. Serikali itaendelea kusimamia misamaha ya kodi, na itatolewa pale itakapoonekana ni yenye tija na kwa mujibu wa Sheria zilizokuwepo.

**Makusanyo halisi Vs Misamaha ya kodi**




## D. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**26. Mheshimiwa spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/22, Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha marekebisho ya Sheria pamoja na Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

**I. Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria zikiwemo:**

i. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Kampuni Namba 15 ya mwaka 2013;

ii. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998;

iii. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995;

iv. Kupunguza Kiwango cha Ushuru wa Forodha ili Kushajihisha Uwekezaji katika Uzalishaji wa Viwanda vya Nguo;

v. Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016;

vi. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009;

vii. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya mwaka 2017;

viii. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Namba 11 ya 2004;

ix. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2006;

x. Kufanya marekebisho ya Kanuni za Ada na tozo ya mwaka 2015; na

xi. Kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Namba 8 ya mwaka 1994.

**II. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi**

i. Kuunganisha Mfumo wa Tehama wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania;

ii. Kuwatambua Wafanyabiashara wa Mtandaoni;

iii. Kuendeleza Mfumo wa Kuwatambua Walipakodi Kimaeneo (Block Management System);

iv. Kuendelea na Ukaguzi wa Kodi katika Taasisi za Fedha na Kampuni za Mawasiliano;

v. Kupata Taarifa za Kodi Kutoka Chanzo cha Tatu;

vi. Kugomboa Madeni ya Kodi; na

vii. Kuongeza Kiwango cha Gawio kutoka Mashirika ya Serikali.

**27. Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya kina ya utekelezaji wa hatua hizo yanapatikana katika **Jadweli namba IV.**

## E. TATHMINI YA DENI LA TAIFA

**28. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2022, Deni la Taifa limefikia jumla ya TZS 1,202.6 bilioni ikiwemo:

### a. Deni linalodhaminiwa na SMZ

**29. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2022, Deni la Taifa linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ni TZS 310.7 bilioni. Deni hilo limeongezeka kwa TZS 76.3 bilioni sawa na ongezeko la 33% ikilinganishwa na deni lililoripotiwa katika mwezi Machi 2021 ambalo lilikuwa TZS 234.4 bilioni.

i. Deni la ndani hadi kufikia Machi 2022 ni TZS 282.3 bilioni ambalo limeongezeka kwa TZS 76.3 bilioni sawa na ongezeko la 37% ikilinganishwa na deni lililorikodiwa katika mwezi Machi 2021 ambalo lilikuwa TZS 206.0 bilioni; na

ii. Deni la nje linalodhaminiwa na SMZ hadi kufikia Machi 2022 ni TZS 28.4 bilioni. Deni hili halikuongezeka kwa kipindi cha mwaka mzima wa tathmini.

**b. Deni la Nje lililokopwa na SMT kwa ajili ya Miradi iliyotekelezwa Zanzibar**

30. **Mheshimiwa Spika,** Deni la nje lililokopwa na SMT kwa ajili ya Miradi iliyotekelezwa Zanzibar limefikia TZS 891.9 bilioni ikiwa na ongezeko la TZS 225.2 bilioni kutoka TZS 666.7 bilioni kwa taarifa zilizotolewa katika mwezi wa Machi 2021.

**c. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Taifa**

31. **Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa lililoripotiwa mwishoni mwa mwezi wa Machi 2022 limeonesha kuwa ni himilivu kwa kuzingatia uwiano ufuatao:

i. Thamani ya deni linalodhaminiwa na SMZ ni TZS. 301.7 bilioni wakati Uchumi wa Zanzibar hadi Disemba 2021 umethaminishwa kwa TZS 4,632.7 bilioni. Hivyo, uwiano wa Deni la Taifa dhidi ya GDP ni 6.5% wakati ukomo wa deni kwa kigezo cha uchumi wa nchi ni 70% kwa nchi za Uchumi wa Kati kwa Kiwango cha Chini.

32. **Mheshimiwa Spika,** Hali halisi inaonesha kuwa Deni la Zanzibar bado ni himilivu na hivyo Serikali inaweza kuendelea kukopa ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

## F. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/2022

33. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya Serikali ifikapo Juni 30 mwaka 2022, mapato ya Serikali yatafikia jumla ya TZS 1,507.0 bilioni sawa na 82% ya makadirio ya mwaka. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 909.7 bilioni sawa na 80% ya makadirio ya awali.

**a. Uchambuzi wa ukusanyaji wa Mapato hadi kufikia Juni 2022**

34. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 733.5 bilioni, sawa na 76.5% ya bajeti ya TZS 959.2 bilioni. Mapato hayo yanaonesha ukuaji wa 17.7% ikilinganishwa na mapato ya TZS 623.4 bilioni yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

35. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) inatarajiwa kukusanya TZS 377.0 bilioni sawa na 72% ya Makadirio ya TZS 525.1 bilioni. Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar inatarajiwa kukusanya TZS 338.9 bilioni sawa na 82% ya Makadirio ya TZS 413.1 bilioni. Aidha, kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT ambao wanafanya kazi Zanzibar inatarajiwa kufikia TZS 17.5 bilioni sawa na 83.3% ya lengo la kukusanya TZS 21.0 bilioni.

36. **Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 176.3 bilioni sawa na 100.3%, ambapo ni sawa na ukuaji wa 76.0% ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato wa TZS 100.2 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita. Mapato haya yanajumuisha: Mapato ya Wizara yanategemewa kufikia TZS 154.3 bilioni sawa na 123.5% ya makadirio ya mwaka ya TZS 124.9 bilioni; Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 13.0 bilioni sawa na 36.4% ya makadirio ya mwaka ya TZS 35.7 bilioni; Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 9.0 bilioni sawa na 60.0% ya makadirio ya mwaka ya TZS 15.0 bilioni.

37. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio hadi kufikia Juni, 2022, Mkopo wa ndani utafikia TZS 140.0 bilioni sawa na 152% ya lengo la TZS 92.00 bilioni. Mikopo hii inajumuisha hati fungani ya muda mrefu ya TZS 20.00 bilioni kupitia minada ya Benki kuu na hati fungani maalum (Special Bond) za mda mrefu iliyo na gharama nafuu ukilinganisha na hati fungani za sokoni zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) zenye thamani ya TZS 120.00 bilioni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

### b. Makusanyo yanayotarajiwa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

38. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa makusanyo kutoka Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia TZS 224.7 bilioni sawa 79% ya makadirio ya kupokea TZS 283.0 bilioni. Makusanyo hayo yanajumuisha TZS 57.0 bilioni (72% ya makadirio ya TZS 79.0 bilioni) ikiwa ni Misaada na TZS 167.70 bilioni (82% ya makadirio ya kukopa TZS 204.0 bilioni) ni Mikopo.

39. **Mheshimiwa Spika,** Makusanyo mengineyo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 232.58 bilioni ikiwemo: Misaada ya Kibajeti ya TZS 2.4 bilioni (12% ya makadirio ya TZS 20.0 bilioni) na TZS 230.18 bilioni ni fedha iliyopokelewa kutoka IMF.

### c. Matarajio ya Matumizi Julai 2021-Juni 2022

40. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kumalizika kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 yanatarajiwa kufikia TZS 1,507.0 bilioni sawa na 82 % ya bajeti ya mwaka yaTZS 1,829.9 bilioni, ambapo jumla ya TZS 739.0 bilioni zitatumika kwa matumizi ya Kazi za Kawaida sawa na 78% na TZS 768.0 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na 87% ya makadirio ya awali kwa mchanganuo ufuatao:

i. Matumizi ya Mishahara yanatarajiwa kufikia TZS 411.8 bilioni ambapo TZS 341.4 bilioni kwa Wizara na Taasisi zenye Mafungu, sawa na 94% ya bajeti ya mwaka na TZS 70.4 bilioni zitatumika kulipa mishahara ya Taasisi zinazopokea Ruzuku, sawa na 92% ya bajeti ya mwaka.

ii. Kwa upande wa Matumizi Mengineyo, jumla ya TZS 144.6 bilioni zinatarajiwa kutumika, ambapo kwa Wizara na Taasisi zenye Mafungu matarajio ni kutumia TZS 97.8 bilioni sawa na 49% ya makadirio ya mwaka, wakati kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku yanatarajiwa kutumia TZS 46.8 bilioni, sawa 48% ya makadirio ya mwaka.

41. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nikiri kwamba kiujumla kwa mwaka 2021/2022 matarajio ya Matumizi Mengineyo ya kuendeshea shughuli za Serikali yamekuwa chini ya lengo kutokana na kuendelea kuwepo kwa changamoto ya ukusanyaji wa mapato zinazotokana na sababu mbali mbali zikiwemo zile za ndani ya nchi pamoja na mabaliko ya kijamii na kiuchumi duniani.

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 182.6 bilioni, sawa na 88% ya makadirio ya mwaka;

iv. Matumizi ya Maendeleo kwa fedha za ndani yanatarajiwa kufikia TZS 372.4 bilioni sawa na 61 ya makadirio ya mwaka; na

v. Matumizi kutokana na fedha zinazotarajiwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 395.6 bilioni, sawa na 143% ya makadirio ya mwaka hii inajumuisha na matumizi ya fedha za Mkopo nafuu kutoka IMF.

## G. MAFANIKIO YA SERIKALI MWAKA 2021-2022

### a. Maendeleo ya Utalii

42. **Mheshimiwa Spika,** Tunafahamu kwamba uchumi wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa unategemea Sekta ya Utalii. Serikali inaendelea kuchukua jitihada mbali mbali ili kukuza maendeleo ya Sekta hii. Kwa kuwa Sekta hii ukuaji wake pia unategemea hali ya Usalama wa Nchi na Dunia. Katika kulisimamia hili na kuhakikisha Sekta hii inakuwa katika hali ya usalama Serikali imeanzisha kikosi kazi maalumu cha Polisi Utalii na Diplomasia ambacho jukumu lake kubwa ni kuhakikisha usalama wa watalii na mali zao wanapokuwa katika maeneo mbalimbali ya kitalii hapa nchini.

43. **Mheshimiwa Spika,** Hadi sasa kikosi hichi kina jumla ya Maafisa Polisi 150 wanaotoka katika vikosi vyetu vya ulinzi na usalama ambao tayari wameshapatiwa mafunzo maalum kwa lugha mbali mbali za Kimataifa pamoja na mafunzo ya Diplomasia ambayo yatarahisisha kutoa huduma kwa watalii pale ambapo itahitajika. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuzindulia rasmi kikosi hichi siku ya tarehe tarehe 19 Novemba, 2021.

44. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga TZS 500 milioni kwa ajili ya kuendesha shughuli za kikosi hichi, Hivyo matumaini yetu kuwa

kuimarika kwa ulinzi na usalama wa watalii wanaotembelea Zanzibar kutaifanya Zanzibar kuwa ni kituo salama cha Utalii na kupelekea kuongezeka kwa watalii kutembelea nchi yetu. Aidha, naomba niunge mkono jitihada za Viongozi wa Wakuu wa nchi yetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maono makubwa ambayo kimsingi yamekuja wakati muafaka.

45. **Mheshimiwa Spika,** Sote ni mashuhuda, hivi karibuni viongozi wetu hawa walivyoshiriki moja kwa moja kuioneshea dunia taswira ya Tanzania ikiwemo maeneo mahsusi ya kiutalii kwa upande wa Zanzibar kupitia "filamu" maalum ijulikanayo kwa jina la **TANZANIA THE ROYAL TOUR.** Tuna imani kubwa kuwa sasa milango ya masuala ya utalii na uwekezaji katika sekta hiyo inakwenda kufunguka zaidi na kuongeza pato letu la taifa na kuongeza ajira kwa vijana wetu. Kupitia filamu hiyo ambayo imeongeza chachu ya kuzitangaza fursa za uwekezaji na maendeleo imeweza kusaidia kupata makumpuni na Taasisi mbali mbali zilizoonesha nia ya kuja na kuwekeza Zanzibar. Ombi langu binafsi, kwa Sekta ambazo zinatoa huduma tujipange ili kukabiliana na neema kubwa inayokuja kutokana na matokea ya filamu hii.

**b. Uchumi wa Buluu**

46. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi za visiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Awamu ya nane chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi imejipanga vyema kutumia fursa zinazohusu matumizi bora ya rasilimali za bahari kwa ajili ya kuimarisha au kukuza uchumi wa nchi yetu. Sekta hii, imeendelea kuimarika hususan baada ya Serikali kuamua kuchukua jitihada za makusudi kuwawezesha wajasiriamali wa Sekta hiyo katika kukuza ubunifu, kuwapatia zana, mitaji na masoko. Hii pia imehusisha pamoja na ujenzi wa miundombinu, kuongeza uzalishaji na uhifadhi ili kuimarisha ubora wa mazao ya baharini. Mikakati hiyo inahusisha ununuzi wa boti 577 kwa ajili ya wavuvi ambazo zitaongeza uwezo wa wavuvi kufika masafa ya mbali. Boti hizo zinatarajiwa kufika mwishoni mwa mwezi wa Juni 2022. Aidha, Serikali imenunua boti ndogo (vihori) 500 kwa ajili ya wakulima wa mwani na hadi kufikia mwezi Mei 2022, jumla ya boti 250(50%) zilikwishapokelewa kutoka kwa wazabuni. Boti hizi zimekakabidhiwa Serikalini na taratibu za kuwakabidhi wajasiriamali wanaojishughulisha na ukulima wa mwani zinaaendelea.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022-2023, Sekta ya Uchumi wa Buluu imetengewa jumla ya TZS 89.66 bilioni ili kutekeleza mpango wa mwaka 2022-2023 ikiwemo Ujenzi wa Bandari mbili za uvuvi kwa jumla ya TZS 30.00 bilioni; Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza maboti na kusarifu samaki vyenye thamani ya TZS 11.00 bilioni; kuanza hatua za awali za kuweka hifadhi ya mafuta TZS 2.00 bilioni na hifadhi ya gesi TZS 4.00 bilioni na Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia taarifa za utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia TZS 5.0 bilioni.

### c. Sekta ya Kilimo

48. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo ni miongoni mwa Sekta tegemezi kwa uchumi wetu wa Zanzibar. Kwa mwaka 2021, Sekta hii imechangia 24%, na inachangia wastani wa 40% ajira kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2021-2022, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya kisasa ili kuepuka utegemezi wa misimu ya mvua katika kilimo. Serikali imeshakamilisha uchimbaji na uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji yenye urefu wa mita 1,400 katika bonde la Mlemele; uwekaji wa pampu katika visima 20 vya mabonde ya Cheju; Kibokwa na Kilombero. Matumaini ya Serikali ni kuwepo kwa miundombinu hiyo kutasaidia kuimarisha uzalishaji wa mazao ya nafaka ikiwemo mpunga na mategemeo ya Serikali ni kuongezeka kwa kipato cha wakulima wetu.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2022-2023, Sekta hii imetengewa jumla ya TZS 53.59 bilioni miongoni mwa shughuli zinazokwenda kutekelezwa ni pamoja kuimarisha huduma za matrekta ili kuweza kutoa huduma kwa wakati kwa mabonde yenye ukubwa wa ekari 9,000 kwa Unguja na ekari 8,400 kwa Pemba kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Sambamba na hilo kwa mwaka ujao Serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde yenye ukubwa wa hekta 370 na kuunga umeme wa njia kubwa bonde la Cheju B.

### d. Sekta ya Usafirishaji

50. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Usafirishaji ni sekta ambayo ni chachu katika kukuza uchumi wetu hapa nchini. Sekta hii inajumuisha, usafiri wa baharini, usafiri wa nchi kavu na usafiri wa Anga. Kwa upande wa usafiri wa baharini tayari Serikali inaendelea na mikakati ya kuendelea na uwekaji wa miundombinu rafiki ili kuruhusu Ujenzi wa Bandari jumuishi itakayojengwa Mangapwani. Aidha, SMZ tayari imekamilisha ujenzi wa Gati ndogo katika Bandari ya Mkokotoni ambayo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa maadhimisho ya Sherehe za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

51. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali kupitia mpango wake wa Uimarishaji Viwanja vya Ndege imekamilisha ujenzi wa Ofisi za Watendaji katika Uwanja wa Ndege wa Nungwi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma. Aidha, Serikali imeingia mkataba na Kampuni ya Kimataifa ya DNATA kwa ajili ya kutoa huduma katika Uwanja mpya wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) ikiwa na lengo la kuimarisha viwango vya huduma kwa wenyeji na wageni wanaotumia uwanja huo kwa shughuli za usafiri ndani na nje ya nchi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2022, Kampuni hiyo ya kimataifa, tayari imeshaleta vifaa mbali mbali vya kisasa vitakavyotumika kuhudumia ndege aina zote zinazowasili Zanzibar.

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023, Serikali inatarajia kutumia Euro 50.0 milioni sawa na TZS 126.30 bilioni ikiwa ni sehemu ya mkopo wa Nje wenye jumla ya Euro 201 milioni kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja Mpya wa Ndege Pemba.

53. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa usafiri wa nchi kavu. Serikali tayari imeanza ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa kilomita 22.1 ambapo kazi hii inatarajiwa kukamilika ndani kipindi cha miaka miwili. Kwa upande wa miundombinu ya barabara za ndani, Serikali imekamilisha maandalizi ya ujenzi wake zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga TZS 135.0 bilioni kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 100 za barabara za Mjini. Pia, Serikali itakopa TZS 202.10 bilioni kwa ajili ya Ujenzi wa barabara za Tunguu-Makunduchi, Fumba-Kisauni, na Chake-Mkoani.

**e. Sekta ya Mawasiliano**

54. **Mheshimiwa Spika,** Kwa wakati huu tulionao, Sekta ya Mawasiliano ina umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha usalama wa mawasiliano kuliko ilivyokuwa wakati mwingine wowote. Miundombinu ya Mawasiliano inapokuwa imara inaweza kuleta mageuzi makubwa mno katika kila nyanja ya maisha yetu, ikiwemo miundombinu muhimu kama vile usafiri na usafirishaji, huduma za kifedha, usambazaji wa umeme, huduma za afya na huduma nyingine nyingi. Kwa kuwa katika nchi yetu Sekta hii inashugulikiwa na pande zote mbili za Muungano, kwa mashirikiano na wenzetu kutoka SMT, Serikali inaendelea kukamilisha zoezi la operesheni ya Anuani za Makaazi na Postikodi na kwa hapa Zanzibar katika Shehia 59, kwa kuwekwa namba za anuani za makaazi pamoja na kusajili taarifa za wakaazi katika Mfumo wa "National Physical Addressing (NaPA)."

55. **Mheshimiwa Spika,** Technolojia ya habari na Mawasiliano ina nafasi kubwa katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kuboresha maisha na kuleta maendeleo kwa wananchi hasa wale wa vijijini, kwa kuwawezesha wakulima kupata masoko ya bidhaa zao, pamoja na kupata huduma mbalimbali za jamii zinazowezesha kuinuwa uchumi kwa akina Mama, vijana na wananchi kwa ujumla. Katika kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinapatikana na kufikiwa katika maeneo yote ya mijini na vijjiini, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imetiliana saini na Kampuni ya Zantel kujenga minara 45 katika maeneo 42 Unguja na Pemba. Ujenzi wa minara hii kutawezesha kuondoa changamoto ya mawasiliano katika maeneo mbali mbali mijini na vijijini. Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga TZS 7.8 bilioni kwa ajili Wakala wa Miundombinu ya Tehama (Zanzibar ICT infra-stracture Agency) ili kusimamia vyema miundombinu ya TEHAMA nchini.

### f. Sekta ya Fedha

56. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Fedha ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa Nchi ambapo, kwa kipindi cha robo tatu kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 sekta hii imeweza kuchangia kwa 3.5% Katika pato la Taifa. Kwa hapa Zanzibar, Sekta ya Fedha inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na taasisi zinazotoa huduma ndogo ndogo za fedha (Microfinance). Sekta ndogo ya benki ndio imechukua nafasi kubwa katika sekta ya fedha, ikishikiliwa na mabenki 14 ambayo yamefunguwa matawi katika maeneo tofauti hapa Zanzibar.

57. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2022, amana zilizopokelewa katika sekta ndogo ya Benki ni TZS 1,501.0 bilioni kutoka TZS 1,098.7 bilioni zilizokuwepo mwishoni mwa mwezi wa Julai 2021. Amana zinazohitajika wakati wowote ni 54% ya amana zote. Aidha, Mikopo iliyotolewa katika kipindi cha Julai hadi Machi 2022 imefikia TZS 747.3 bilioni ikiwa na ongezeko la TZS 209.80 bilioni ikilinganishwa na TZS 537.5 bilioni zilizokopeshwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Mikopo iliyoelekezwa katika biashara imechukua 14% ya mikopo yote, ikifuatiwa na 11.4% iliyoelekezwa katika sekta ya Utalii, 9.8% imeelekezwa katika mikopo binafsi na kiwango kilichobakia kilielekezwa katika Sekta nyengine za kiuchumi.

58. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwepo mabenki makubwa yanayotoa huduma kwa wananchi bado kuna eneo kubwa la wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakitumia huduma za kifedha zinazotolewa na taasisi ndogo ndogo za fedha (Microfinance Institutions). Hadi kufikia Machi 2022, idadi ya taasisi zilizosajiliwa na kupewa kibali cha kutoa huduma Zanzibar zimefikia nne (4) ikiwemo: BRAC Zanzibar finance Ltd; Vision Microcredit Ltd; ASA Microfinance Zanzibar-Ltd na TAQWA Microfinace Ltd. Serikali inatambua uwepo wa Taasisi hizi na pia imekua ikithamini mchango mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu. Sambamba na mchango unaotolewa bado kuna changamoto kubwa ya sekta ndogo ya "microfinance" kuvamiwa na baadhi ya wawekezaji ambao hawana nia njema kwa wananchi wetu. Wamekua wakitumia taasisi hizi kwa kunufaisha maslahi yao binafsi na kuathiri hali za maisha ya wananchi wetu. Aidha, riba zinazotozwa kwa wananchi ambao hutumia huduma zinazotolewa ni kubwa na hazina malengo ya kuwasaidia wananchi badala yake zimekua zikileta taharuki kwa nchi na wananchi. Hivyo, Serikali inawatahadharisha wananchi kuwa makini na taasisi zinazotoa huduma hizo. Hadi ninasoma hotuba hii Taasisi zilizoruhusiwa ni hizo nilizozitaja na kuanzia mwaka 2022-2023, OR-Fedha na Mipango imeandaa utaratibu wa kila mwezi kuzitangaza taasisi hizi ambazo zitaruhusiwa kutoa huduma ya kukopesha. Iwapo, taasisi itatoa huduma na haimo katika orodha itakayotolewa, nawaomba sana wananchi wetu kutoa taarifa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

**59. Mheshimiwa Spika;** Matarajio kuwa Sekta ya fedha itaimarika kwa kiwango kikubwa kufuatia kuimarika kwa shughuli za biashara na uwekezaji duniani na maboresho yanayoendelea kutekelezwa baina ya SMZ na SMT katika sekta hii. Aidha, katika kuongeza wigo wa matumizi ya Sekta ya Fedha (Financial Inclusion), kwa mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imedhamiria kuimarisha matumizi ya huduma ndogo ndogo za fedha nchini. Serikali itatoa muongozo maalum wa usajili na ufuatiliaji kwa Taasisi zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili kuimarisha usimamizi pamoja na kuongeza wigo wa utoaji wa huduma hizo kwa Wananchi. Pia, uanzishwaji wa huduma na bidhaa mpya za kifedha (financial product) zinazoambatana na imani (Islamic financial products) za wananchi wengi zitasaidia sana kukuza Sekta hii kwa Zanzibar.

**g. Sekta ya Nishati**

**60. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukua kila aina ya jitihada ili kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo yote wanapata huduma za nishati kulingana na mahitaji yao. Kwa mwaka 2021-2022, idadi ya wananchi waliojitokeza kuomba na kuunganishiwa umeme Unguja na Pemba imeongezeka kufikia wateja wapya 19,823 na kuweza kupeleka umeme katika vijiji 22 Unguja na 14 Pemba. Vilevile Serikali imezifanyia matengenezo laini kubwa za umeme zenye mkondo wa kilovolti 33 pamoja na kubadilisha nguzo mbovu 450 kwa Unguja na 1,050 kwa Pemba. Pamoja na kuimarisha miundombinu mengine ili kuwa na huduma ya uhakika ya upatikaji wa Umeme kwa nchi yetu. Aidha Serikali inaendeleza Mikakati ya kupeleka umeme mbadala katika maeneo ya visiwa ikiwemo visiwa vya Kokota na Njau.

**61. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya nane chini ya Uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, imedhamiria kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inakuwa ni rafiki, yenye uhakika na endelevu kwa mwaka 2022-2023, Serikali imeshafunga mkataba na Benki ya Dunia na itatumiaTZS 17.79 bilioni ikiwa sehemu ya mkopo wa USD 150 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi na Kuibadilisha Sekta ya Nishati Zanzibar (Zanzibar Energy Sector Transformation and Accessibility ZESTA). Matumaini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa kukamilika kwa mradi huu kutapelekea kuimarika kwa huduma za upatikanaji umeme Zanzibar.

**62. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa nishati za mafuta, Serikali imekua ikitumia Mifumo mbali mbali ili kudhibiti bei za bidhaa hizi na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa nishati hiyo inakuwa endelevu. Kufuatia vita vya Ukraine na Urusi vilivyoanza mwezi wa Februari 2022, bei za upatikanaji wa nishati za mafuta zimekuwa zikipanda kwa kasi kubwa na kuashiria kuathiri harakati za uchumi kiujumla. Ili kukabiliana na hilo, Serikali imelazimika kupunguza kodi ya Mfuko wa Miundombi kutoka TZS 100 hadi TZS 50 kwa lita ya Petroli na Diseli na kupunguza leseni ya Barabara (road licence) kutoka TZS 38 hadi TZS 15 kwa lita ya Petroli na Diseli. Aidha, Serikali ilipunguza kodi ya Mfuko wa Maendeleo ya Barabara (Road Development Fund) kutoka TZS 100 hadi TZS 70 kwa lita

ya Petroli, Tozo la Petrol kutoka TZS 350 hadi TZS 300 kwa lita ya Petroli. Yote haya yamefanyika kwa lengo la kudhibiti upandaji wa bei kwa nishati ya mafuta ili kupunguza athari za mfumuko wa bei za mafuta katika masoko yetu ya ndani na kuwapa nafuu ya maisha wananchi wetu.

**h. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

63. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Mikakati mbali mbali ya nchi yetu ikiwemo Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2020-2025 ambapo katika ibara 142 imeelekeza kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupambana na umasikini bado. Serikali inaendeleza azma yake ya kuwawezesha wananchi kuwa sehemu ya wazalishaji mali na watoa huduma kwa ajili ya kuinua kipato cha mtu binafsi na kunyanyua Uchumi wa nchi yetu. Hivyo, Serikali ya Awamu ya nane imedhamiria kutekeleza Ilani yetu ya CCM kwa vitendo. Hili limedhihirika tarehe 26/ 11/2021 katika maadhimisho ya kutimiza mwaka mmoja wa Utawala na Uongozi wa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi alipoeleza mipango mipana ya Serikali juu ya kuwanyanyua na kuwawezesha Wajasiriamali wadogo wadogo.

64. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia fedha zilizopatikana kutoka Mkopo wa IMF, Serikali imetenga fedha kwa makundi mbali mbali ili kuwawezesha kupata Mitaji na maeneo ya kufanyia biashara ili nao iwe sehemu ya uzalishaji katika jamii ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza utegemezi na kukuza uchumi wetu. Aidha, Serikali iliingia katika makubaliano maalum na Benki ya CRDB ili kuwapatia mitaji kwa njia ya Mkopo ambayo haitakuwa na gharama wala riba katika upatikanaji wake. Lengo na madhumuni ni kuwawezesha wananchi kupata fedha kwa gharama nafuu ili kuendeleza biashara na shughuli za ujasiriamali. Hadi kufikia Mei, 2022, CRDB wameshakamilisha taratibu za mikopo yenye thamani TZS 4.944 bilioni kwa ajili ya vikundi 602 ambavyo vimetimiza vigezo na masharti yaliyowekwa. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tuendelee kuwahamasisha wananchi katika maeneo yetu kutumia fursa hii ili kufikia lengo lililowekwa. Matarajio ya Serikali ni kwamba iwapo mikopo hii itatumika vyema basi itatengeneza ajira zaidi ya 100,000 hivyo, si vyema tukapoteza fursa hii.

65. **Mheshimiwa Spika,** Sote, Tunafahamu Serikali ya Awamu ya Nane wakati inaingia madarakani ilikumbana na changamoto kubwa ya wananchi wake kutapeliwa na Kampuni maarufu ijulikanayo kwa jina la Masterlife Microfinance Ltd iliyosajiliwa kwa biashara ya ufugaji na uuzaji wa mifugo ya ndege (Poltry) Tanzani Bara na kuja kufanya kazi hapa Zanzibar. Ni wazi kuwa suala lile liliathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wetu wakiwemo Wajasiriamali ambao kwa kiasi kikubwa ndio wahanga wa kadhia hiyo. Kwa mantinki hiyo hiyo iliyoelezwa Ibara ya 142 ya Ilani yetu ya Uchaguzi wa CCM 2020-2025, Serikali iliamua kuwarejeshea Amana wananchi waliopeleka fedha zao katika Kampuni hiyo ya Masterlife Microfinance ltd. Hadi Machi 2022, wananchi 9,264 wenye mikataba yenye thamani ya TZS 23.77 bilioni wameshalipwa

ambapo Serikali imechangia TZS 16.98 bilioni. Mheshimiwa Spika, haya yote yamekwenda kukwamua zile changamoto za uchumi zilizosababishwa kutokana na kukosekana kwa mitaji ya kuendesha biashara.

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imedhamiria kuwa na programu maalum ya kutoa taaluma juu ya masuala ya fedha na uwekezaji (financial literacy Campaign), ili wananchi waweze kufahamu njia na utaratibu sahihi za kuwekeza fedha pamoja na viashiria vitakavyopelekea kupoteza fedha zao kwa njia za kudanganywa kuwekeza na kupata faida. Hii pia itajumuisha, zile mbinu zinazotumika kukusanya fedha katika mitandao.

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kujenga uwezo Vijana katika rika tofauti ili waweze kujiajiri katika Sekta binafsi badala ya kusubiri ajira kutoka Serikalini ambazo kwa kawaida hazitoshelezi. Kwa mwaka 2020-2021, Serikali imewawezesha vijana 6,131 ikiwemo 5,700 ndani ya nchi na 431 nchi za nje ikiwemo Oman, Qatar, UAE, Syshelles, Maldives, Kuwait, Yemen na Saudi Arabia. Aidha, Serikali imeendelea kufuatilia ili kuhakikisha ulipaji wa mishahara katika Sekta binafsi unaendana na maelekezo ya Serikali, hivyo kwa mwaka 2020-2021, Serikali imefanya ukaguzi maalum kwa taasisi 232 na imebaini taasisi 19 kati ya hizo zilikuwa hazifuati muongozo wa ulipaji ya mishahara wa kima cha chini. Mheshimiwa Spika, Nichukue fursa hii kuwakumbusha waajiri wote kufuata Sheria za Kazi ipasavyo na kuacha visingizio vyovyote ili kukwepa kulipa kima hicho.

**i. Sekta ya Uwekezaji**

68. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kisera na kisheria ili kuimarisha uwekezaji wa ndani na nje nchini ambao utaweza kuongeza pato la taifa, kukuza ajira, uchumi wa nchi pamoja na kuleta maendeleo endelevu yatakayo imarisha ustawi wa wananchi bila ya kuharibu mazingira, silka, mila na tamaduni nzuri za Wazanzibari. Serikali kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imefanikiwa kusajili miradi ya uwekezaji 81 ukilinganisha na usajili wa miradi 63 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 likiwa ni ongezeko la miradi 18. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Miradi hiyo inatengeneza mtaji wa makisio ya dola za kimarekani 1.02 bilioni ukilinginisha na dola za kimarekeni 336.4 milioni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikiwa ni sawa na ongezeko dola za Kimarekani zipatazo 683.7 milioni.

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 miradi ya uwekezaji inatarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 5,000 kwa wananchi. Katika kuweka mkazo kwenye shughuli za uwekezaji, kusaidia kukuza ajira na kuchangia uchumi, Serikali imetangaza visiwa kumi (10) kwa ajili ya uwekezaji na tayari wameshajitokeza wawekezaji kwa visiwa hivyo. Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 261.5 zinatarajiwa kukusanywa zikiwa ni malipo ya awali. Pia, Serikali

imeanza mchakato wa kutangaza visiwa vyengine 9 kwa Uwekezaji ambapo visiwa 6 tayari wameshajitokeza wawekezaji na matarajio ni kukusanya malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Kimarekani 5.8 milioni. Miongozo ya uhifadhi wa mazingira na ushiriki wa wananchi,ikiwemo: Suala la urudishaji wa Uwekezaji kwa jamii husika (Corporate Social Responsibility) ili kuwezesha uchumi endelevu katika visiwa hivyo imeandaliwa na imekamilika.

70. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka ujao wa fedha 2022/2023 Serikali inatarajia kupokea na kusajili miradi ipatayo zaidi 90 ambayo itatengeneza mtaji wa dola za Kimarekani zipatazo 1.6 bilioni na kuleta ajira zipatazo 6,000 kwa wananchi.

**j. Sekta ya Elimu**

71. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ikiwa ni nchi yenye amani, jamii yake inahitaji kupata elimu bora. Hivyo, kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikiekeza katika elimu kama njia ya kukabiliana na changamoto za kimaendeleo. Sekta ya elimu ina mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii yetu. Kwa mwaka 2021-2022, Sekta hii imepata mafanikio kwa kuimarika kwa miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa na madawati.

72. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kusambaza seti za madawati 5,342 Unguja na 6,000 Pemba ya wanafunzi katika Skuli za Sekondari Unguja na Pemba; ukamilishaji wa madarasa 103 na kuzifanyia ukarabati skuli 36 pamoja na kukamilisha ujenzi wa vyoo 114 Unguja na Pemba; kuufanyia marekebisho mfumo wa elimu kwa kurejesha darasa la saba katika ngazi ya elimu ya msingi. Sambamba na hilo Serikali imefanikiwa kuwapatia chakula wanafunzi 14,437 wa Skuli 27 za Msingi katika Wilaya saba za Unguja na Pemba kupitia Mradi wa Lishe.

73. **Mheshimiwa Spika,** Tunakumbuka kwamba Serikali ilitenga TZS 69 bilioni zilizopatikana kwa mkopo wa IMF na kuelekezwa katika kuimarisha miundombinu ya elimu ikiwemo:

i. Ujenzi wa madarasa 805 (madarasa 425 ya kukamilishwa ambayo yaliyoanzishwa na wananchi, madarasa 380 ni madarasa mapya). Tayari madarasa ya Mfano yamekamilika katika maeneo yote ya ujenzi na sasa Wakandarasi wanandelea kukamilisha madarasa mengine katika meneo mbalimbali ya Unguja na Pemba;

ii. Ujenzi wa Skuli 10 zikiwemo 8 za ghorofa 2 za chini. Skuli za ghorofa zinajengwa katika maeneo ya Kwabitihamrani msingi, Kidongochekundu msingi, Mtopepo sekondari na Kwa Pemba ni Maeneo ya Pujini Sekondari, Kwale msingi, Mwambe msingi na Makangale sekondari.

**74. Mheshimiwa Spika,** Sasa yale mabati ambayo yamezingizwa na yamekuwa kero kwa baadhi ya wananchi wetu tunawaomba kuendelea kuwa wastahamilivu kwani dhana yake sasa imeshaanza kudhihirika, ambapo matunda yake tunatarajia kuanza kuyatumia muda mfupi ujao.

**75. Mheshimiwa Spika,** Pia Serikali kupitia mradi huu imenunua skuli moja ya Sekondari katika maeneo ya Bweleo ambayo kazi za umaliziaji zinaendelea. Skuli mbili za chini ni za msingi za elimu mjumuisho katika eneo la Jendele kwa Unguja na Pujini kwa Pemba. Pamoja na kujenga Vyoo 1,693 katika skuli mbalimbali za Unguja na Pemba. Kupitia, fedha hizo Serikali inakarabati Skuli 25 Unguja na Pemba. Aidha, kazi za uchongaji wa madawati 4,012 yenye thamani ya TZS 2.00 bilioni.

### k. Upatikanaji wa Maji Safi na Salama

**76. Mheshimiwa Spika,** Sote tunafahamu kuwa, Maji yana umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku mwanandamu na uendeshaji wa shughuli muhimu za kiuchumi na kijamii. Hali ya upatikanaji wa maji safi na salama inaendelea kuimarika katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Mamlaka ya Maji Zanzibar imechukua hatua kubwa ya kuikarabati miundombinu mipya ya maji. Kwa mwaka 2021, Serikali imefanya utanuzi na ukarabati wa mtandao wa maji kwa kulaza mabomba kwa eneo lenye ukubwa wa kilomita 5.6 Unguja na kilomita 2.7 Pemba. Kupitia, matumizi ya fedha zilizopatikana kwa mkopo wa IMF zilizoelekezwa katika Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar tayari utekelezaji wake umeanza ambapo uchimbaji wa visima 35 kati ya visima 64 vinavyotarajiwa kuchimbwa umekamilika pamoja na ujenzi wa matangi ambao hadi sasa umefikia wastani wa asilimia 40. Sambamba na hili, kazi za ulazaji wa mabomba kwa mradi mzima imekamilika kwa wastani wa kilomita 64. Imani yetu ni kwamba ujenzi wa miundo mbinu utakapokamilika utapunguza tatizo la maji kwa 71%.

**77. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga TZS 106.73 bilioni kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma za Maji Safi na Salama-Zanzibar. Sekta ya Maji imekuwa ikikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo Mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yameathiri vyanzo vyetu vya maji na kupelekea kukauka ama kuwa na viwango visivyofaa (maji kuwa na chumvi) kwa matumizi ya maji. Aidha, kuharibika kwa miundombinu ambayo inahitaji fedha nyingi katika kurekebishwa nalo husababisha changamoto ya ukosefu wa huduma hii kwa wananchi wetu.

**78. Mheshimiwa Spika,** Kwa kudhibiti changamoto hizi Serikali imeamua kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Maji ili kuwa na rasilimali za uhakika kwa ajili ya kukabiliana na kazi za Ujenzi na Matengenezo endelevu ya Miundombinu ya maji.

## l. Sekta ya Afya

**79. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi wote. Serikali inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake kwani afya bora ni raslimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana na Wizara kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022 ni pamoja na: Kukamilika kwa muongozo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma; Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Nne wa Wizara; Kukamilika kwa mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini(Monitoring & Evaluation Framework);Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Taarifa za Afya; Kuvuka malengo ya dunia ya kufikia shabaha ya 90 tatu katika mapambano ya UKIMWI; Kukamilika kwa hospitali ya wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu; na Kukamilika kwa jengo la maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa huko Mombasa;

**80. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia fedha za IMF inaendelea na ujenzi wa hospitali 10 za wilaya na hospitali moja (1) ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Mpaka kufikia Machi 2022 ujenzi wa hospitali hizi umefikia 50%. Lengo kuu la ujenzi wa hospitali hizi ni kufikisha huduma za afya karibu na wananchi pamoja na kupunguza msongamano katika hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Hadi kukamilika kwake ujenzi wote unategemewa kutumia kiasi cha TZS 60.15 bilioni na TZS 21.45 bilioni zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, gari za kubebea wagonjwa na gari za kusambazia dawa.

**81. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga jumla ya TZS 188.22 bilioni. Majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na: Kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya; Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za chanjo ili kudhibiti maradhi yanayozuilika kwa chanjo; Kuimarisha utoaji wa huduma shirikishi za UKIMWI, Kifua Kikuu, Homa ya Ini na Ukoma; Kuimarisha huduma za afya ya Mama na Mtoto ili kupunguza magonjwa na vifo;Kujenga hospitali mpya ya wagonjwa wa akili eneo la Kinyasini Pemba na hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo la Mahonda;Kujenga kituo cha damu salama Pemba; Kuanzisha utaratibu maalum wa utoaji wa huduma za afya kwa watalii; Ununuzi wa vifaa vya maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa;Kuendelea kutoa huduma za kibingwa ikiwemo usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo, uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya satarani (chemotherapy), huduma za ubongo na uti wa mgongo; Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa pamoja na upatikanaji wa huduma za matibabu ya rufaa; Kuendelea na Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Hospitali ya Chake Chake; Ujenzi wa nyumba za Wafanyakazi Hospitali ya Abdalla Mzee na shughuli nyengine ambazo zimewasilishwa katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya 2022-2023 ya Wizara ya Afya.

## H. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022.

**82. Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar utaendelea kuimarika na kufikia ukuaji wa wastani wa 5.4 % kutoka ukuaji wa wastani wa 5.1% kwa mwaka 2021. Ukuaji huu utachangiwa na mikakati ifuatayo:

i. Kudhibiti kasi ya Mfumko wa bei na kubaki ndani ya wigo wa 3%-5% chini ya 5% kwa viwango vya Kikanda,

ii. Kuimarika kwa Uwekezaji, biashara na utalii ikiwa ni matokeo ya faida ya filamu ya Tanzania Royal Tour;

iii. Utekelezaji wa Sera za Kodi na bajeti pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara;

iv. Kudhibiti matumizi ya Serikali na upotevu wa mapato kutokana na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji mapato na kuimarisha udhibiti wa matumizi ili kuelekeza matumizi hayo katika shughuli za kiuchumi na kijamii;

v. Kukuwa kwa Sekta ya fedha kufuatia maboresho yanayoendelea kutekelezwa katika sekta ya fedha ikiwemo matumizi ya teknolojia na ubunifu katika utoaji wa huduma za fedha; hatua zinazochukuliwa katika kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza viwango vya riba.

## I. SERA NA MIKAKATI YA SERIKALI ILIYOTUMIKA KWA MATAYARISHO YA BAJETI 2022-2023

**83. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022-2023, tutaendeleza jitihada, maono na juhudi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwenye kuimarisha Usimamizi katika matumizi ya fedha za Umma na kuelekeza rasilimali hiyo katika kutekeleza miradi ya kimkakati itakayowanyanyua na kuwaunganisha wananchi pamoja na kudumisha umoja wa kitaifa. Bajeti ya mwaka 2022-2023 imejikita katika utekelezaji wa Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo 2050, Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2020-2025, Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar 2021-2026 (ZADEP); na Mpango wa mwaka 2022-2023 ambao niliuwasilisha mbele ya Baraza lako leo asubuhi.

**84. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mikakati ya nchi, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) itaendelea kutekeleza Mikakati ya Kimataifa na ile ya Kikanda. Hivyo, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Bajeti ya mwaka 2022-2023 hii imezingatia mikakati mahsusi ya Kikanda na imebeba Kauli mbiu ya **Kuongeza Kasi ya Kufufua Uchumi na Kuimarisha Maisha ya Wananchi.** Kutokana na kauli mbiu hiyo, Bajeti ya mwaka 2022-2023 imeweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo:

i. **Kuimarisha huduma za jamii;** Kwa kuimarisha sekta ya afya, elimu na maji pamoja na utekelezaji wa miradi inayoendelea na uanzishwaji wa miradi mipya. Jumla ya TZS 588.61 bilioni zimetengwa ili kuimarisha huduma za kijamii na kuimarisha maendeleo ya mwanadamu (Human Development);

ii. **Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika utoaji wa huduma za Serikali**. Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imepanga kuimarisha matumizi ya Mifumo na kiumarisha taasisi za usimamizi wa Mifumo ya Serikali ikiwemo Wakala wa Serikali Mtandao na Wakala wa Miundombinu ya Tehama. Taasisi hizi kwa ujumla zinatarajiwa kutumia TZS 12.10 bilioni ili kuendelea na utoaji wa huduma za Mifumo ya Kielektroniki kwa Serikali;

iii. **Kuimarisha maslahi ya Watumishi wa Umma**. Kwa mwaka 2022-2023, Serikali imetenga TZS 628.68 bilioni sawa na 24% ya Bajeti kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi ikiwemo na marekebisho mapya ya mishahara kama ambavyo imeleekezwa na Serikali. Pia Serikali imejipanga kuanza rasmi kutoa mishahara kwa Madiwani wa Wadi ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kusimamia wananchi katika Wadi zao kwa ufanisi zaidi. Pia, Serikali imedhamiria kuanzisha fao la kupoteza ajira ambalo litasimamiwa chini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

iv. **Kutekeleza miradi ya kimkakati**. Kupitia Mpango wetu wa muda wa Kati, Serikali imepanga kuanza utekelezaji wa miradi 13 ya kimkakati ambayo itabadilisha taswira ya Zanzibar, kukuza uchumi na kuimarisha huduma za jamii na kuongeza fursa za ajira ambapo jumla ya TZS 798.19 bilioni zimetengwa ili kutekeleza miardi hiyo;

v. **Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili na kupambana na udhalilishaji**. Serikali itaendelea kuimarisha taasisi za usimamizi wa haki za binaadamu kwa kuweka miundombinu rafiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa taasisi hizo;

vi. **Kuendelea kuitangaza Zanzibar kiutalii**. Kwa lengo la kuimarisha Sekta mama ya Utalii nchini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuzitumia vyema fursa za Uwekezaji zinazotokana na matunda ya ukanda wa "TANZANIA ROYAL TOUR" ili kukuza vitega uchumi na kuendelea kuzalisha ajira kwa vijana wetu;

## I. HATUA ZITAKAZOCHUKULIWA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**85. Mheshimiwa Spika,** Serikali imechukua hatua kadhaa za kuweka mfumo wa kodi ulio tulivu na wenye kutabirika, kushajiisha ulipaji wa Kodi kwa hiari, kukuza ajira na kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na

kuchochea kasi ya ukuaji wa Uchumi. Aidha, hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni zile zinazohusu marekebisho ya Sheria pamoja na zinazohusu kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

86. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima naomba uniruhusu kuziwasilisha kama ifuatavyo:

**I. Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria**

**a. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya mwaka, 1998**

**Moja**: **Kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Mashine za kieletronik za kutolea Risiti na karatasi za kuchapishia Risiti**

87. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuongeza wigo wa matumizi wa mashine za kutolea risiti ili kupunguza gharama, kushajiisha na kuhamasisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwa kutolea risiti za mauzo ya biashara. Serikali inapendekeza kufuta kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Mashine za Kielektroniki na karatasi za kutolea risiti wakati wa uingizaji na usambazaji (uuzaji) kwa mawakala wa uingizaji na usambazaji walioteuliwa na Serikali.

**Pili: Kuimarisha Huduma za Utoaji wa Mikopo kwa Benki za Kiislamu (Islamic Bank)**

88. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto za utozaji Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) mara mbili kwa Benki za Kiislam, ambapo kodi hutozwa wakati wa Benki inaponunua bidhaa na wakati wa kuwasilisha bidhaa hiyo kwa mteja. Hivyo, ili kuimarisha Huduma za Utoaji wa Mikopo kwa Benki za Kiislamu (Islamic Bank), Serikali inapendekeza kufuta kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wakati Benki inapowasilisha bidhaa kwa mteja ili kubainisha kuwa mikopo mbadala iliyoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) inayotolewa na benki kwa wateja wake ambayo inahusisha ununuzi na uuzaji wa mali anazozihitaji mteja kwa faida inayowekwa juu ya gharama ya mali ni sawa na mikopo mingine ya kawaida.

89. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hii haimwondolei muuzaji wajibu wa kulipa kodi ya ongezeko la thamani la mtaji kwa mujibu wa sheria katika muamala wa mauzo ya mali kwa mteja wa benki aliyenunua mali hiyo kupitia utaratibu wa mkopo mbadala. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa Wazanzibari wote wanaweza kupata mikopo kwa unafuu katika Taasisi za Fedha ikijumuisha wale ambao hawakubaliani na utaratibu wa "riba".

**Tatu: Utozaji wa Kodi kwenye Huduma zitolewazo Mitandaoni**

90. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya SMT na SMZ zimefanya mazungumzo na Kampuni zinazomiliki mitandao ya kijamii ili kuangalia utaratibu mzuri wa kutoza

Kodi ya Mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika biashara za huduma zinazotolewa mtandaoni (Digital Services). Aidha, hatua hii inalenga kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipakodi wanaotoa huduma za kidijitali bila ya kuwa na makazi hapa nchini. Kwa mwaka wa fedha ujao 2022/23, Serikali inapendekeza kuanza kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa huduma zinazotolewa mtandaoni. Jumla ya TZS 6.0 bilioni zinatarajiwa kukusanya kutokana na hatua hii.

**Nne: Kuingizwa katika Wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) watoa Huduma za Kitaalamu (Professional Services Providers)**

**91. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeko la biashara ya watoa huduma za kitaalamu (Professional Services Providers) pamoja na kukosekana kwa taarifa sahihi za biashara hizo. Serikali inapendekeza Kuingizwa katika wigo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa watoa huduma za kitaalamu waliosajiliwa na Bodi za Kitaalamu (Professional Body) ili kupata taarifa sahihi pamoja na kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Jumla ya TZS 1.5 bilioni zinatarajiwa kukusanya kutokana na hatua hii.

**Tano: Kuimarisha uchumi wa ndani kwa kushajiisha Wawekezaji kununua bidhaa ndani ya nchi.**

**92. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 inapendekeza kuongeza unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka aslimia 80 hadi 100 kwa Mwekezaji asiyekuwa wa Kimkakati (Non-Strategic Investor) wakati wa ununuzi wa bidhaa nchini kwa ajili ya ujenzi. Aidha, hatua hiyo itakwenda sambamba na marekebisho ya kupunguza unafuu wa VAT kutoka asilimia 80 hadi asilimia 75 wakati wa uingizaji wa bidhaa nchini.

**b. Sheria ya Ushuru wa Stempu nambari 7 ya mwaka 2017.**

**Moja: Kuweka usawa wa malipo ya Ushuru wa Stempu kwa wafanyabiashara Wadogo wadogo.**

**93. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022-2023,Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria wa Ushuru wa Stempu kwa kurekebisha jadweli namba 2 ili kuleta usawa (Equity) katika ulipaji wa Ushuru wa Stempu kwa Wafanyabiashara wadogo wadogo kwa mujibu wa mauzo ghafi kwa mwaka kama inavyoonekana katika Jadweli, hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS. 3.5 bilioni.

**94. Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba kuitafsiri kama ifuatavyo: Mauzo yasiozidi TZS 5.0 milioni hatapaswa kulipia; Mauzo baina TZS 5.0 milioni hadi TZS 7.50 milioni atatozwa TZS 100,000 **(Laki moja tu); Mauzo** yasiozidi TZS 7.50 milioni hadi TZS 10.0 milioni atatozwa TZS 200,000 (Laki mbili tu); Mauzo baina ya TZS 10.0 milioni hadi TZS 12.50 milioni atatozwa

TZS 300,000 (Laki tatu tu); na Mauzo baina ya TZS 12.50 milioni hadi TZS 15.0 milioni atatozwa TZS 400,000 (Laki nne tu).

| MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA SHERIA YA USHURU WA STAMPU NAM. 7 YA 2017 | | |
|---|---|---|
| **S/N** | **KIWANGO CHA MAUZO TZS** | **MALIPO KWA MWAKA** |
| 1 | Mauzo yasiyozidi TZS 5,000,000. | NILL |
| 2 | Mauzo yanayozidi TZS 5,000,000 hadi 7,500,000 | 100,000 |
| 3 | Mauzo yanayozidi TZS 7,500,000 HADI 10,000,000 | 200,000 |
| 4 | Mauzo yanayozidi TZS 10,000,000 hadi 12,500,000 | 300,000 |
| 5 | Mauzo yanayozidi TZS 12,500,000 hadi TZS 15,000,000 | 400,00 |

**Pili: Kupunguza viwango vya Ushuru wa Stempu katika Gari za biashara**

95. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuwepo kwa uwajibikaji mdogo kwa Walipakodi wanaofanya biashara za gari uliotokana na viwango vya kutozea Ushuru wa Stempu. Kwa mwaka 2022-2023, Serikali inapendekeza kupunguza viwango vya kutozea Ushuru wa Stempu kwa gari za biashara kwa 25% ili kuongeza uwajibikaji, ulipaji kodi wa hiari, pamoja na kuleta ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**c. Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabarani Namba. 7 ya mwaka 2003**

96. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeona kuna haja ya kurahisha usajili wa vyombo vya moto, Hivyo inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabarani Nam. 7 ya mwaka 2003 kama ifuatavyo:

i. Kupunguza ada ya usajili wa nambari binafsi kutoka TZS 15 milioni kwa miaka mitano hadi TZS 5 milioni kwa miaka mitatu ili kuhamasisha wananchi kuweza kuitumia fursa hii na kuongeza mapato ya Serikali; na

ii. Kupandisha ada za usajili wa vyombo vya moto kwa asilimia ishirini (20%) ili kuweza kuendana na mabadiliko ya hali ya sasa. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo: Kutoka TZS 108,420 hadi TZS 130,000 kwa vyombo vya maringi manne; Kutoka TZS 61,950 hadi TZS 75,000 kwa maringi mawili; na Kutoka TZS 56,020 hadi TZS 67,000 kwa vyombo vyenye uwezo wa engine capacity zaidi ya 50.

d. **Marekebisho ya Sheria ya Tozo ya Petroli namba. 7 ya mwaka 2001.**

**Kujumuisha utaratibu wa utozaji wa Gesi asilia katika Tozo la Petroli.**

97. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha udhibiti wa mapato yatokanayo na bidhaa ya gesi asilia, Serikali inapendekeza kuondosha utaratibu wa utozaji Ushuru wa Stempu kwa bidhaa ya gesi asilia na badala yake kuweka utaratibu wa kutoza tozo la petroli katika bidhaa hiyo wakati wa uingizaji nchini kama ilivyo katika utaratibu wa kutoza kodi za mafuta. Hatua hiyo itasaidia kupatikana kwa makusanyo sahihi, kuondosha usumbufu kwa wafanyabiashara wa rejareja pamoja na kudhibiti bei ya bidhaa hiyo.

e. **Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba. 12 ya mwaka 2016.**

**Kutayarisha Kanuni za miongozo ya Utoaji wa Misamaha ya Kodi**

98. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Serikali inatarajia kutoa kanuni ya miongozo ya utoaji wa misamaha ya kodi ili kusimamia, kudhibiti pamoja na kuongeza ufanisi katika utowaji wa misamaha ya kodi.

f. **Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi Nambari 7 ya Mwaka 2009.**

**Kutayarisha Kanuni za miongozo ya Uwekaji wa dhamana katika uendeshaji wa biashara.**

99. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ukwepaji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wa hoteli wanapoondoka nchini kutokana na kutolipa madeni ya kodi, hali hii inatokana na kukosekana kwa kanuni zinazotoa miongozo ya uwekaji wa dhamana ("security") katika uendeshaji wa biashara hizo.

100. **Mheshimiwa Spika,** Ili kurekebisha kasoro hiyo, kwa mwaka wa fedha 2022/23, Serikali inatarajia kutayarisha Kanuni za miongozo ya Uwekaji wa dhamana katika uendeshaji wa biashara hiyo ili kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali.

g. **Sheria ya kukuza uwekezaji Zanzibar namba 14 ya mwaka 2018**

**Kushajiisha uzalishaji wa ndani kwa wawekezaji wa kimkakati kwa kutoa unafuu wa malighafi wakati wa uingizaji.**

101. **Mheshimiwa Spika,** Ili kushajiisha uwekezaji katika sekta ya viwanda vya ndani kwa wawekezaji wa kimkakati (strategic investor), Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa malighafi (raw material) na pembejeo za viwandani (industrial input) wakati wa uingizaji.

**h. Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

**Kutoza Kodi ya Miundombinu katika Vinywaji vikali na Sigara**

**102. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2022/23, Serikali inapendekeza kuanza kutoza Kodi ya Miundombinu kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vinywaji vikali na sigara wakati wa uingizaji nchini (importation & transfer). Aidha, kianzio hicho kitajumuishwa katika vianzio vya Kodi ya Miundombinu, ambapo asilimia 50 ya mapato yatatumika kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa miundombinu nchini na asilimia 50 iliyobaki itatumika kama chanzo cha mapato katika Mfuko wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Uchumi (Econimic Stabilization Fund). Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla TZS 3.5 bilioni.

**II. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi**

**Moja: Uunganishaji wa Mifumo ya Forodha (TANCIS), Usajili wa Gari (MVLRS) na Mfumo wa VFMS.**

**103. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha ujao 2022/23, Serikali itaunganisha Mifumo wa Forodha (TANCIS), Usajili wa Gari (MVLRS) na mfumo wa VFMS ili kudhibiti usajili wa gari zinapoingia nchini, kupata takwimu sahihi za Ankara za kodi (input tax) kwa waingizaji (importer) pamoja na kufatilia mwenendo wa walipakodi ili Mamlaka za Usimamizi wa Kodi (TRA&ZRB) ziweze kufanya makadirio sahihi ya kodi. Jumla ya TZS 4.2 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na hatua hii.

**Pili: Kuanza kukusanya kodi ya mapato kwa Kampuni za kigeni za usafirishaji (non - resident person)**

**104. Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar imekuwa haikusanyi Kodi ya Mapato ya 5% kwa kampuni za kigeni za usafirishaji wa abiria na mizigo. kwa mwaka wa fedha ujao 2022/23 TRA – Zanzibar itaanza rasmi kukusanya kodi hiyo kupitia wakala wa Shirika la Meli na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 1.3 bilioni.

**Tatu: Kuzitaka Kampuni za Kigeni (Foreign Company) Zilizosajiliwa Nje ya Zanzibar kuwasilisha Hesabu za Kifedha (Fanancial Statements) kwa Wakala wa Usajili wa Biashara (BPRA)**

**105. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka fedha 2022/23 Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) itasimamia ipasavyo uwasilishaji wa Hesabu za Kifedha (Fancial Statements) kwa Kampuni zilizosajiliwa Nje ya Zanzibar na zinafanya Biashara hapa Zanzibar. Aidha, takwa hilo kwa mujibu wa kifungu cha 242 cha Sheria ya Makampuni namba 15 ya mwaka 2013.

## J. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.


### a. Makadirio ya Mapato Serikali kwa mwaka 2022/2023

**106. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia taarifa ya mwenendo na muelekeo wa Hali ya Uchumi iliyotolewa, Mapato ya Serikali kwa mwaka 2022-2023, yanakadiriwa kufikia Jumla ya TZS 2,590.30 bilioni. Uchambuzi wake ni kama ufuatavyo:

i. TZS 1,369.75 bilioni sawa na 53% ya makisio ya mwaka 2022-2023 ambazo zinakadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani zikiwemo TZS 135.7 bilioni ambazo ni marejesho ya fedha zilitumika kulipia Ujenzi wa Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege wa AAKIA (Terminal III);

ii. TZS 687.95 bilioni sawa na 27% zitatokana na Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambazo zimejumuisha: Mikopo TZS 606.86 bilioni ambapo imejumuisha TZS 126.3 bilioni zimeelekezwa katika ujenzi wa Uwanja Mpya wa Ndege utakaojengwa Pemba, TZS 202.1 bilioni kwa ajili ya Ujenzi wa barabara za Tunguu-Makunduchi, Fumba-Kisauni, na Chake-Mkoani, TZS 279.0 bilioni zimeelekezwa katika miradi mbali mbali ya kisekta; TZS 10 bilioni zinatokana na msaada wa kibajeti; na TZS 71.08 bilioni ni Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

iii. Mikopo ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Miradi ya kimkakati zinakadidiriwa kufikia jumla ya TZS 515.0 bilioni sawa na 20% ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2022-2023 (TZS 400.00 bilioni zinatokana na mikopo itakayokopwa ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) na Mikopo ya muda mfupi (Hati Fungani) ni TZS 115.00 bilioni;




iv. TZS 17.60 bilioni zinakadiriwa kukusanywa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa sawa na 1% ya mapato yanayokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2022-2023.

107. **Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Mwelekeo wa Bajeti umeambatanishwa katika Mapendekezo ya Sura ya Bajeti ya mwaka wa Fedha 2022/2023 yanayopatikana katika **Jadweli namba. III.**


**b. Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/2023**

108. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo na mwelekeo wa Uchumi mwaka 2022, Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamekadiriwa kutumia jumla ya TZS 2,590.30 bilioni ambayo mgao wake ni kama ifuatavyo:

i. TZS 1,220.51 bilioni sawa na 46.98% zimeelekezwa kwa matumizi ya kawaida ikiwemo: Matumizi ya mshahara kwa wafanyakazi wa Serikali ni TZS 628.68 bilioni; Matumizi mengineyo ya Uendeshaji ni TZS 381.53 bilioni; Mfuko Mkuu wa Serikali ni TZS 210.3 bilioni;

ii. TZS 682.54 bilioni sawa na 26.42% ni fedha itakayotolewa na SMZ kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ikiwemo: Ujenzi wa kilomita 100 wa barabara za mjini pamoja na miundombinu yake; Ujenzi wa Mji wa Serikali; Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya; na Programu ya Kuimarisha Miundombnu ya Elimu (Mageuzi ya Elimu);

iii. TZS 669.65 bilioni sawa na 25.92% ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambazo zimepangwa kutekeleza program na Miradi ya maendeleo ikiwemo Ujenzi wa Uwanja wa ndege mpya wa Pemba na Ujenzi wa barabara 3 kubwa ikiwemo: Barabara ya Tunguu-Makunduchi, Kisauni-Fumba na Chake Chake-Mkoani; Boosting Inclusive Growth for Zanzibar (BIG-Z); Zanzibar Energy Sector Transformation and Access Process (ZESTA); Tanzania Social Action Fund (TASAF); Uimarishaji na Uhuishaji wa Maji safi na salama Zanzibar na mengineyo imewasilishwa katika Mpango wa mwaka 2022-2023;



iv. Matumizi kwa Serikali za Mitaa yanakadiriwa kufikia TZS 17.60 bilioni sawa na 0.68% ya matumizi yote ya Serikali (Tanbihi: Ikumbukwe kwamba matumizi haya hayajumuishi Mishahara ya watumishi wa Serikali za Mitaa.)

**c. Mfuko wa Miundombinu**

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2022-2023 Serikali imetenga jumla ya TZS 28.6 bilioni kwa ajili ya matumizi ya Mfuko wa miundombinu katika miradi maalum ikiwemo: Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, Ujenzi wa Uwanja Mdogo wa Kigunda, Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani na Mradi wa Kuifanyia mabadiliko Sekta ya Nishati.

**d. Hali ya Utegemezi kwa mwaka 2022/2023**

**110. Mheshimiwa Spika,** Hali ya Utegemezi wa Bajeti ya Zanzibar inaendelea kushuka kutoka asilimia 4.3 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia asilimia 2.7 kwa mwaka huu wa Fedha 2022/2023. kutokana na kupungua kwa Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka huu wa Fedha tunatarajia kupokea TZS 71.09 bilioni ukilinganisha na makadirio ya matumizi ya TZS 2,590.3 bilioni. Mgawanyo wa Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi unaoneonekana katika **Jadweli namba III.**

## K. SHUKRANI

**111. Mheshimiwa Spika,** Kwa Niaba ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango naomba kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupatia ambayo yanaimarisha Muungano wetu. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maendeleo na wale waliochangia Bajeti yetu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 zikiwemo Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Jamhuri ya watu wa China, Korea ya Kusini, Kuwait, Malaysia, Misri, Norway, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Uingereza, Marekani Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu. Pia nayashukuru mashirika na Taasisi zifuatazo : Africa Development Bank (AfDB), Global Fund (GF), BADEA, IFAD, , KOICA, ,UNDP, UNICEF, World Bank (WB), Exim Bank, Global Partner Ship for Education(GPE), United State Agency for International Development (USAID), United Nation Population fund (UNFPA), Saudi Fund (SF), United Nation For Women (UN Women), Khalifa Fund (KF), Global Fund (GF), Korea, MILELE NORAD, UNESCO, Partnership for Child Development International Atomic Energy Agency(IAEA) na United Nation Environment Programme (UNEP).

**112. Mheshimiwa Spika,** Sasa nawashukuru viongozi wote wa OR-Fedha na Mipango akiwemo Naibu Waziri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Muwakilishi wa Jimbo la Pangawe Mhe. Ali Suleiman Ameir. Pia ninamshukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dkt. Juma Malik Akil kwa uratibu na usimamizi mzuri wa Maandalizi ya bajeti hii akifuatiwa na Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Dkt Rahma Mahfoudh, Naibu Makatibu Wakuu Fedha na Mipango

Bwana Aboud Hassan Mwinyi na Bwana Rashid Said Rashid na watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango itifaki imezingatiwa. Nawashukuru sana jinsi tunavyoshirikiana kutekeleza majukumu ya Serikali yetu.

113. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipekee nawashukuru waandisi ambao wanaofuatilia mchakato mzima wa matayarisho ya Bajeti pamoja na wananchi wanaotufuatilia kupitia vyombo hivyo. Mheshimiwa Spika, nikiwa naelekea katika hitimisho la Hotuba yangu natoa rai kwa wananchi wenzangu tuendelee kuimarisha umoja wetu na tusijali itikadi za kisiasa, dini wala ukabila. Tuendelee kufanya kazi kwa ufanisi na uaminifu na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji.

114. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu, naomba kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya jitihada zake anazozichukua katika kuhamasisha ukusanyaji wa mapato. Hivyo, sote tuwe mabalozi wazuri juu ya hili na naomba kunukuu kauli yake aliyoitoa katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika mwisho wa mwezi wa Mei 2022 na kusisitiza kuwa **"Kila mtu unaponunua chochote ni wajibu wetu kudai risiti tena risiti ya mashine (EFD). Hiyo ndio itakayopelekea Serikali kuweza kupata kodi ya kufanya haya tunayoyafanya".**

## L. HITIMISHO

115. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishie Serikali kwa mwaka wa fedha, 2022/2023 kukusanya jumla ya TZS 2,590.30 bilioni ( Shilingi trilioni mbili bilioni mia tano na tisiini na milioni mia tatu). Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani ni TZS 1,369.75 bilioni, Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo TZS 687.95 bilioni, Mikopo ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo ni TZS 515.0 bilioni. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha TZS 17.60 bilioni kukusanywa na Serikali za Mitaa.

116. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 2,590.30 bilioni (Shilingi trilioni mbili bilioni mia tano na tisiini na milioni mia tatu) ambapo TZS 1,220.51 bilioni zimeelekezwa kwa ajili ya kazi za kawaida,TZS 1,352.19 bilioni zimeelekezwa kwenye kutekeleza Mpango wa Maendeleo; na TZS 17.60 bilioni zinakwenda kutumika katika Serikali za Mitaa.

117. **Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

Dkt. Saada Mkuya Salum
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**

| JADWELI NAM.I | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MAPATO | Juni, 2022. | | | | |
| | | | | | Tarakimu ni "Bilioni" |
| MAELEZO | BAJETI 2021/22 | JULAI -MACHI 2021 | | | |
| | | Makadirio | Halisi | %Bajeti | %miezi 9 |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***1,134.90*** | ***902.02*** | ***675.76*** | **60%** | **75%** |
| ZRB | 525.10 | 414.85 | 275.20 | ***52%*** | ***66%*** |
| TRA | 413.10 | 306.70 | 256.36 | ***62%*** | ***84%*** |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 175.70 | 164.80 | 130.90 | ***75%*** | ***79%*** |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.00 | 15.67 | 13.30 | ***63%*** | ***85%*** |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | ***283.00*** | ***207.20*** | ***119.58*** | **42%** | **58%** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 13.50 | | | | |
| Ruzuku kutoka Nje | 65.50 | 54.20 | 37.14 | ***57%*** | ***69%*** |
| Mkopo kutoka Nje | 204.00 | 153.00 | 82.44 | ***40%*** | ***54%*** |
| ***Mapato Mengineyo*** | ***412.00*** | ***340.18*** | ***332.48*** | **81%** | **98%** |
| Mkopo wa Ndani | 92.00 | 100.00 | 100.00 | ***109%*** | ***100%*** |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 220.00 | | | | |
| Mkopo wa shirika la fedha la dunia (IMF) | | 230.18 | 230.18 | | ***100%*** |
| Marejesho ya Mkopo | 80.00 | | | | |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 20.00 | 10.00 | 2.30 | ***12%*** | ***23%*** |
| ***Jumla Kuu*** | ***1,829.90*** | ***1,449.40*** | ***1,127.82*** | **62%** | **78%** |
| **MATUMIZI** | | | | | |
| ***Matumizi ya Kawaida*** | ***947.10*** | ***670.35*** | ***565.99*** | **60%** | **84%** |
| Mshahara Mawizara | 364.90 | 256.09 | 256.09 | ***70%*** | ***100%*** |
| Mshahara Ruzuku | 76.80 | 52.80 | 52.80 | ***69%*** | ***100%*** |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 200.20 | 147.30 | 85.03 | ***42%*** | ***58%*** |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 97.50 | 66.18 | 35.13 | ***36%*** | ***53%*** |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 207.70 | 147.98 | 136.95 | ***66%*** | ***93%*** |
| ***Matumizi ya Maendeleo*** | ***882.80*** | ***371.20*** | ***301.61*** | **34%** | **81%** |
| Fedha za Serikali | 606.50 | 158.56 | 88.97 | ***15%*** | ***56%*** |
| Mkopo wa Shirika la Fedha la Dunia (IMF) | | 96.39 | 96.39 | | ***100%*** |
| Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 276.30 | 116.25 | 116.25 | ***42%*** | ***100%*** |
| ***Jumla Kuu*** | ***1,829.90*** | ***1,041.55*** | ***867.60*** | **47%** | **83%** |
| ***Chanzo:*** *Afisi ya Rais- Fedha na Mipango* | | | | | |

| JADWELI NAMBA II | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2022/2023-2024/2025 | | | | | | |
| Tarakimu ni TZS "bilioni" | | | | | | |
| **A: MAPATO** | | | | | | |
| **MAELEZO** | **Makisio 2021/22** | **Matarajio 2021/22** | **% ya Bajeti** | **Makadirio 2022/23** | **Makisio 2023/24** | **Makisio 2024/25** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,134.9** | **909.7** | **80%** | **1,234.10** | **1,413.0** | **1,635.3** |
| ZRB | 525.1 | 377.0 | **72%** | 579.50 | 645.8 | 724.3 |
| TRA | 413.1 | 338.9 | **82%** | 454.10 | 519.9 | 590.8 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 175.7 | 176.3 | **100%** | 179.50 | 226.3 | 299.2 |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.0 | 17.5 | **83%** | 21.00 | 21.00 | 21.00 |
| **Mapato ya ODA** | **363.0** | **224.7** | **62%** | **813.60** | **688.7** | **658.2** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 13.5 | | | 0.23 | | |
| Ruzuku kutoka Nje | 65.5 | 57.0 | **87%** | 70.81 | 17.1 | 14.7 |
| Mkopo kutoka Nje | 204.0 | 167.7 | **82%** | 606.86 | 671.6 | 643.5 |
| Marejesho ya Mkopo (EXIM BANK OF CH | 80.0 | - | **0%** | 135.70 | | |
| **Mapato Mengineyo** | **332.0** | **372.6** | **112%** | **525.00** | **520.0** | **625.0** |
| Mkopo wa Ndani /TB | 92.0 | 140.0 | **152%** | 115.00 | | |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maende | 220 | - | | 400.00 | 500.0 | 600.0 |
| Mkopo wa IMF | - | 230.2 | | | | |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 20 | 2.4 | **12%** | 10.00 | 20.0 | 25.0 |
| **Jumla Kuu** | **1,829.9** | **1,507.0** | **82%** | **2,572.70** | **2,621.7** | **2,918.5** |
| **B:UKOMO WA MATUMIZI** | | | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **947.1** | **739.0** | **78%** | **1,220.51** | **1,255.3** | **1,310.7** |
| Mshahara Mawizara | 364.9 | 341.4 | **94%** | 557.95 | 520.5 | 550.2 |
| Mshahara Ruzuku | 76.8 | 70.4 | **92%** | 70.73 | 87.5 | 89.0 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 200.2 | 97.8 | **49%** | 265.38 | 277.3 | 280.8 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 97.5 | 46.8 | **48%** | 116.15 | 132.0 | 140.2 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 207.7 | 182.6 | **88%** | 210.30 | 238.0 | 250.5 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **882.8** | **768.0** | **87%** | **1,352.19** | **1,359.4** | **1,600.8** |
| Fedha za Serikali | 606.5 | 372.4 | **61%** | 682.54 | 670.7 | 942.6 |
| Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 276.3 | 395.6 | **143%** | 669.65 | 688.7 | 658.2 |
| **Jumla Kuu** | **1,829.9** | **1,507.0** | **82%** | ***2,572.70*** | **2,614.7** | **2,911.5** |
| ***Chanzo: Afisi ya Rais- Fedha na Mipango*** | | | | | | |

| JADWELI NAM.III | | | |
|---|---|---|---|
| | **SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023** | | |
| | | **Tarakimu ni Bilioni** | |
| | **MAPATO SERIKALI KUU** | | |
| **A** | **Mapato ya Ndani** | | **1,369.75** |
| | Makusanyo ya Kodi upande wa ZRB | 579.51 | |
| | Makusanyo ya Kodi upande wa TRA | 454.06 | |
| | Makusanyo yasiyokuwa ya Kodi | 179.48 | |
| | Makusanyo ya Kodi za Wfanyakazi kutoka SMT (PAYE) | 21.00 | |
| | Fedha itakayorudishwa na EXIM BANK CHINA | 135.70 | |
| **B** | **Misaada na Mikopo Kutoka kwa washirika wa Maendeleo** | | **687.95** |
| | MIsaada ya Kibajeti | 10.00 | |
| | Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 70.86 | |
| | Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta | 606.86 | |
| | Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (Basket Fund) | 0.23 | |
| **C** | **Mikopo ya Ndani na Nje Kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi wa Maendeleo** | | **515.00** |
| | Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 400.00 | |
| | Mikopo ya Hati Fungani | 115.00 | |
| | **JUMLA YA MAPATO YA SERIKALI KUU (A+B+C)** | | **2,572.70** |
| | | | |
| **D** | **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | |
| | **Mapato ya Tozo na Ada** | **17.60** | |
| | **JUMLA YA MAPATO MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA(D)** | | **17.60** |
| | **JUMLA KUU(A+B+C+D)** | | **2,590.30** |
| | | | |
| | **MATUMIZI SERIKALI KUU** | | |
| **E** | **Matumizi ya Kawaida** | | **1,220.51** |
| | Mshahara Mawizara | 557.95 | |
| | Ruzuku za Mishahara | 70.73 | |
| | Matumizi Mengineyo Mawizara | 265.38 | |
| | Ruzuku za Matumizi Mengineyo | 116.15 | |
| | Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | 210.30 | |
| **F** | **Matumizi ya Miradi ya Maendeleo** | | **1,352.19** |
| | Fedha inayotoka Serikalini kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo | 682.54 | |
| | Mikopo kwa Washirika wa Maendeleo | 606.86 | |
| | Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 62.79 | |
| | **JUMLA MATUMIZI YA SERIKALI KUU(E+F)** | | **2,572.70** |
| | | | |
| **G** | **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | **17.60** |
| | **Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani** | **17.60** | |
| | **JUMLA YA MATUMIZI MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA(G)** | | **17.60** |
| | **JUMLA KUU YA MATUMIZI (E+F+G)** | | **2,590.30** |
| | *Chanzo: Ofisi ya Rais Fedha na Mipango* | | |

Jaduweli Nam. IV

**UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

## A. Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria

| S/N | MAREKEBISHO YA SHERIA | MAELEZO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **i.** | **Kufanya marekebisho katika Sheria ya Kampuni Namba 15 ya mwaka 2013** | Kampuni kutoka Tanzania Bara Kuchangia katika Uchumi wa Zanzibar kwa Kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar. | Sheria ya kampuni namba 15 ya mwaka 2013 imerekebishwo ili kuwezesha Kampuni kutoka Tanzania Bara kuchangia katika uchumi wa Zanzibar kwa kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar ambapo watakuwa wanafanya biashara zao. Hadi kufikia Machi jumla ya kampuni 45 kutoka Tanzania Bara tayari zimesajiliwa na zinalipa kodi ya mapato Zanzibar. |
| | | Kuzuia Uhaulishaji wa Hisa na Dhamana Bila ya Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance Certificate). | Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka sharti la kuwasilisha Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance Certificate) wakati wa uhaulishaji kabla ya kubadilisha umiliki wa Hisa na Dhamana. Utekelezaji wake umeanza rasmi Julai, 2021 |
| **ii.** | **Kufanya marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998** | Kuondoa ulipaji VAT Mara Mbili baina ya Tanzania Bara na Zanzibar | Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani imefanyiwa marekebisho na Kanuni ya kutoa muongozo wa marejesheano ya kodi imeanzishwa kwa ajili ya kodi zilizolipwa wakati wa uingizaji bidhaa Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Hadi kufikia Machi, 2022 jumla TZS 24.219 bilioni tayari zimekusanywa na ZRB. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kuongeza Muda kwa Ankara ya Kodi Kuruhusiwa Kupunguza VAT kutokana na Manunuzi | Sheria namba 4 ya mwaka 1998 imefanyiwa marekebisho na kupelekea wafanyabiashara kuwasilisha Ankara kwa wakati. Utekelezaji wa wake umeanza rasmi Julai, 2021. |
| **iii.** | **Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995** | Kufuta Viwango Maalum (specific rates) vya Ushuru wa Hotel | Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995 imefanyiwa marekebisho kwa kufuta Jadweli lililowekwa viwango maalum. Hadi kufikia Machi, 2022 Jumla ya hoteli 219 zilikuwa zimesajiliwa kulipa kiwango maalum (USD 8 na USD5), kati ya hoteli hizo, hoteli 38 zimeshahamishiwa katika wigo wa VAT na hoteli 181 zimehamishiwa katika ulipaji wa ushuru wa hoteli asilimia 12. |
| | | Kuweka Utaratibu wa Utozaji Ushuru wa Hoteli kwa Nyumba za Kulala Wageni zinazotumia Jukwaa la "Airbnb". | Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995 imefanyiwa marekebisho kwa kuweka utaratibu wa utozaji wa ushuru wa Hoteli kwa nyumba za kulala wageni zinazotumia jukwaa la Airbnb. Hadi kufikia Machi, 2022 Jumla ya nyumba 91 zimefanyiwa utambuzi katika maeneo ya Nungwi, Paje, Jambiani na Bwejuu na kusajili jumla ya nyumba 26, na kuingizwa katika wigo wa kodi. |
| **iv.** | **Kupunguza Kiwango cha Ushuru wa Forodha ili Kushajihisha Uwekezaji katika Uzalishaji wa Viwanda vya Nguo** | Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 | Ushuru wa Forodha kwenye malighafi yenye HS Code 5402.33.00 inayotumika kutenegenezea nguo umepunguzwa kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "duty remission" kufuatia Legal Notice iliyotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki Julai, 2021. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 | Ushuru wa Forodha kwenye malighafi zenye HS Code 5407.71.00, 3402.90.00, 3506.91.00, 3208.20.00 na 3208.90.00 zinazotumika kwenye kutengeneza nguo umepunguzwa kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "duty remission" kufuatia Legal Notice iliyotolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki Julai, 2021. |
| **v.** | **Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016** | Kuanza Kukusanya Mapato ya Serikali kwa Kutumia Mfumo Mpya wa Kielektroniki Ujulikanao kama "ZanMalipo" | Sheria husika imerekebishwa na kwa sasa Serikali imeanza kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa ZanMalipo ambapo jumla ya Taasisi 34 zimeunganishwa katika mfumo huo. |
| **vi.** | **Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009** | Kudhibiti Ufungaji wa Biashara na Hesabu za Benki za Walipakodi | Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 imefanyiwa marekebisho kwa kuzuia ufungaji wa biashara na hesabu za benki za walipakodi, isipokuwa kwa idhini ya Kamishna kwa maandishi. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021 |
| | | Kuweka Adhabu kwa Wanufaika wa Misamaha ya Kodi, Watakapoitumia Kinyume na Malengo | Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 imefanyiwa marekebisho kwa kuweka adhabu kali kwa wanufaika hao ikiwa ni pamoja na kulipa kodi iliyosamehewa, kulipa adhabu ya asilimia 50 ya kodi stahiki na kuzuiliwa kupewa msamaha siku za usoni. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kuongeza Kiwango cha Adhabu kwa Wasiotoa Risiti. | Sheria namba 7 ya mwaka 2009 imefanyiwa marekebisho kwa kuweka adhabu ya TZS 2 milioni kwa kila muamala kwa wafanyabiashara ambao hawatoi risiti. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |
| | | Kuondoa Sharti la Malipo ya Awali ya Asilimia 25 ya Kodi Wakati wa Kulipa Kodi kwa Utaratibu wa Awamu | Marekebisho ya sheria namba 7 ya mwaka 2009 yamefanyika kwa kufuta sharti la kulipa asilimia 25 ya kodi na hivyo kuwarahisishia walipakodi kulipa madeni yao kwa wakati. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| vii | **Kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya mwaka 2017** | Kutoa unafuu wa Ushuru wa Stempu kwa Wafanyabiashara Wadogo na Wakati | Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya mwaka 2017 imefanyiwa marekebisho kwa kuwapunguzia mzigo wa kodi na kuwaongezea kipato wafanyabiashara hao. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |
| vii | **Kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Namba 11 ya 2004** | Kupunguza Viwango vya Kodi ya Mapato (Income Tax) kwa Wafanyabiashara Binafsi na Wafanyakazi. | Sheria ya Kodi ya Mapato Namba 11 ya 2004 imefanyiwa marekebisho na utekelezaji wake umeanza rasmi Agosti, 2021. Kiwango cha kodi ya mapato kwa wafanyakazi (PAYE), kimeshuka kutoka asilimia 9 mpaka asilimia 8 na kupandisha kiwango cha chini cha utozwaji kodi (threshold) kutoka 180,000 mpaka 270,000. |
| ix. | **Kufanya marekebisho katika Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2006** | Kuweka Muda Maalum kwa Bodi na Baraza la Rufaa za Kodi kutoa Maamuzi ya Rufaa za Kodi | Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2006 imefanyiwa marekebisho ili kurahisisha maamuzi ya pingamizi, ambapo ndani ya siku 60 baada ya pingamizi husika kusikilizwa maamuzi yatatolewa. Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |
| x. | **Kufanya marekebisho ya Kanuni za Ada na tozo ya mwaka 2015** | Kufuta Tozo ya Biashara (Trade Levy) | Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kufuta Tozo la Biashara (Trade Levy). Utekelezaji wa hatua hii umeanza rasmi Julai, 2021. |
| xi. | **Kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Namba 8 ya mwaka 1994** | Kuzuia Uhaulishaji wa Ardhi, Majengo na Hisa Bila ya Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance Certificate) | Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka sharti la kuwasilisha Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance Certificate) wakati wa uhaulishaji kabla ya kubadilisha umiliki wa ardhi na majengo. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na TRA imetoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhusu utekelezaji wa sheria husika. |

## B. Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria

| S/N | MKAKATI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| i. | **Kuunganisha Mfumo wa Tehama wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania.** | Bodi ya Mapato Zanzibar wamefanikiwa kupata "access"ya kutumia mfumo wa ***TANCIS*** kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na kufanya mafunzo ya pamoja ya jinsi ya kuutumia mfumo huo. Aidha, ZRB imewasilisha *"Concept Note"* kwa TRA ili kutafuta namna bora ya kuinganisha mifumo mengine ya kodi, na TRA wameahidi kufanyia kazi mahitaji hayo. |
| ii. | **Kuwatambua Wafanyabiashara wa Mtandaoni** | Hatua za kukusanya taarifa za wafanyabiasharawa mtandaoni ikiwemo jina la mmiliki, mahali biashara zilipo pamoja na nambari zao za simu zimeshaanza. Aidha, wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar tayari wamekwisha patiwa mafunzo ya "Taxation on digital economies" ili waweze kukusanya kodi kwa wafanyabiashara wa mitandaoni. |
| iii. | **Kuendeleza Mfumo wa Kuwatambua Walipakodi Kimaeneo (Block Management System)** | Hadi sasa ZRB imewatambua walipakodi kwa maeneo yao ya biashara katika mfumo mpya wa utoaji risiti za kielektroniki (VFMS), ambapo Jumla ya walipakodi 604 wameshajiliwa katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Aidha, kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), zoezi la Survey linaendelea kwa kuwashirikisha masheha wote ambao wapo katika maeneo ya mjini, kusini na kaskazini ili kuweza kusajili wafanyabiashara ambao bado hawajafikiwa. Hata hivyo, TRA imefanya zoezi la mlango kwa mlango ili kutoa elimu ya kodi na kuwatambua walipakodi. |
| iv. | **Kuendelea na Ukaguzi wa Kodi katika Taasisi za Fedha na Kampuni za Mawasiliano** | Hadi kufikia Machi, 2022 ZRB imefanya ukaguzi katika kampuni tano, za mawasiliano; 4 kati ya hizo zimeshakamilika na moja inaendelea na iko katika hatua ya mwisho, ambapo Jumla ya TZS 662.65 milioni zimekusanywa kutoka Kampuni ya Zantel. Aidha, kwa upande wa Taasisi za kifedha ZRB katika mwaka wa fedha 2021/2022 itashirikiana na TRA. |

| | | |
|---|---|---|
| **v.** | **Kupata Taarifa za Kodi Kutoka Chanzo cha Tatu** | ZRB na TRA kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali wameweza kupata taarifa za walipakodi ambao hawajasajiliwa na mifumo ya kodi ili kuingizwa katika wigo wa kulipa kodi stahiki. |
| **vi.** | **Kugomboa Madeni ya Kodi** | Hadi kufikia Februari, 2022 makadirio yalikuwa ni kukusanya madeni yenye thamani ya TZS 17.5 bilioni ambapo jumla ya TZS 15.8 bilioni zimegombolewa, sawa na asilimia 90. |
| **vii.** | **Kuongeza Kiwango cha Gawio kutoka Mashirika ya Serikali** | Ofisi tayari imeshawajuilisha mashirika ya Serikali yanayofanya faida kuhusu mabadiliko ya asilimia ya malipo ya gawio kutoka asilimia 20 hadi 50 ya faida inayopatikana kwa mwaka. Aidha, mashirika yote yameshaanza utaratibu wa kutoa gawio hilo kwa Serikali kwa utaratibu uliwekwa isipokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kutokana na tathmini iliyofanywa na Benki Kuu ya Tanzania ambayo imeonesha hajakidhi vigezo na matakwa ya kulipa asilimia 50 ya gawio. Hadi Machi, 2022 jumla ya TZS 5.8 bilioni zimelipwa. |